KIJITABU CHA USHIRIKA
WA
KANISA LA MNAZARETI

Neville Bartle

KIMETAFSIRIWA NA:

Mch. Geofrey Kamando
Rev. Wellington Obotte
Mch. Edson Joseph

KIJITABU CHA USHIRIKA

CHA

KANISA LA MNAZARETI

Church Members Handbook
Kiswahili

Kitabu cha Ushirika
Cha
Kanisa la Mnazareti

Kitabu cha Mwongozo cha Kanisa la Mnazareti 2009 – 2013 kimerahisishwa na kufupishwa na Neville Bartle.

Wachapishaji wa Kimataifa
Wa
Kanisa la Mnazareti

Kimechapishwa na
Kanisa la Mnazareti
S.L.P 16973
Suva, Fiji

Kimetolea na kusahihishwa kwa ruhusa na
Wachapishaji wa Afrika Nazareni
S.L.P 1288
Florida
1710
Afrika Kusini

ISBN 978-0-7977-1185-3

Yaliyomo

Thamani za Kiini…… 6

Utangulizi ……... 8

Kanuni za Imani …… 9

Sheria za Washirika wa Kanisa …….. 18

Ahadi za Mienendo ya Kikristo …….. 21

Uongozi wa Kanisa …….. 29

Kanisa la Mtaa ……. 30

Kikao Kikuu ……. 49

Utumishi Katika Kanisa la Mnazareti …….. 53

THAMANI ZA KIINI
ZA
KANISA LA MNAZARETI

Thamani za Kiini ni muhtasari wa thamani muhimu za Kanisa la Mnazareti.

Sisi ni Watu Wakristo, tuliounganishwa na waumini wa kweli katika kumtangaza Yesu Kristo kama Bwana. Tunaamini kwamba upendo wa Mungu ni mkubwa sana hata akamtoa Mwanawe wa pekee, Yesu awe Mwokozi wetu. Tunaamini kwamba kwa sababu ya dhabihu ya kifo cha Yesu, watu wote waweze kupokea msamaha wa dhambi na kurudishwa katika uhusiano mwema na Mungu. Kwa vile tumepatanishwa na Mungu, tunaamini kwamba ni lazima pia tupatanishwe na kila mmoja. Tunapaswa kupenda kila mmoja kama vile tumependwa na Mungu, na kusamehe kila mmoja kama vile tulivyosamehewa na Mungu. Tunakubali Biblia Takatifu kama chanzo cha ukweli wa kiroho. Sisi ni wa tamaduni Takatifu ya Wesley na tunathibitisha kanuni za kihistoria na itikadi za imani ya Kikristo.

Sisi ni Watu Watakatifu, tulioitwa na Maandiko na kuongozwa na neema kumwabudu Mungu na kumpenda na moyo wetu wote, nafsi na nguvu zetu, na kuwapenda majirani kama vile tunavyojipenda. Tunaamini kwamba kufuatia imani yetu, Roho Mtakatifu huanza kubadilisha na kututia nguvu siku baada ya siku kuwa watu wa upendo na nidhamu ya kiroho, elimu ya maadili, na usafi wa kimaadili, huruma na haki. Ni kazi ya Roho Mtakatifu ambayo inaturudishwa kwa mfano wa Mungu na kuzaa sifa za Kristo. Utakatifu katika maisha ya waumini unaeleweka wazi kama kufanana na Kristo.

Sisi ni watu tilio na misheni ya kuwafanya wanafunzi kama Kristo… kuenenda katika ulimwengu wote. Misheni yetu inaanza

tunapokusanyika pamoja na kisha inaenea katika ulimwengu wote.

Misheni yetu ni kuwapokea waumini wapya katika ushirika na kuanza mikutano mpya ya kuabudu.

Misheni yetu ni kushiriki upendo wa Mungu kwa wale waliopotea na huruma yake kwa maskini na waliovunjika kwa kusaidia kukutana na mahitaji ya watu wanaoumia. Tumejitoa kwa kuwaalika watu kwa imani, kwa kuwajali walio na mahitaji na kuhusisha katika ushirika wetu wale wote watakaoliita jina la Bwana.

Tumejitoa kufundisha na kuelimisha ili wanaume na wanawake wajengwe kama viongozi Wakristo kutimiliza utumishi ambao Mungu ametuitia.

KIJITABU CHA USHIRIKA
KWA
KANISA LA MNAZARETI

Utangulizi

Kijitabu hiki ni mwongozo wa kuwasaidia washirika wa Kanisa kuelewa jinsi Kanisa la Mnazareti linavyoendesha shughuli (kazi) zake. Katiba rasmi ya Kanisa la Mnazareti ni Kitabu cha Mwongozo *(Manual).* Manual ndio kitabu cha kisheria (katiba) na imeandikwa kwa uwazi na maelezo marefu. Watu wengi huona maelezo yaliyomo yana maneno ya kiufundi na magumu kuyaelewa. Kijitabu hiki kinaeleza kwa lugha rahisi mambo muhimu yanayohusu Kanisa la mtaa na shughuli za kiwilaya ya kikanisa. Mambo yote yaliyoandikwa kwenye mabano yanaendeleza kwa mtu kuweza kusoma sehemu hiyo kwenye Manual ili kupata maelezo zaidi.

Utume Mkuu (Manual p 62)

Kazi ya Kanisa la Mnazareti ni kuwajulisha watu wote neema ya Mungu inayobadilisha maisha kupitia msamaha wa dhambi na utakaso wa roho katika Yesu Kristo. Utume wetu, kwanza na zaidi ya yote, ni "kufanya wengine kuwa wanafunzi". Kuwashirikisha waumini katika uanachama na ushirika wa Kanisa na kuwaandaa au kuwatayarisha kwa huduma kwa njia ya mafundisho kwa wote wanaoitikia kwa imani. Lengo kuu ni kuona watu wanajengwa katika kuishi maisha ya utakatifu yanayompendeza Mungu.

Ni katika Kanisa la mtaa ambapo watu wanaokoka, wanafundishwa wanahimizwa na kukuzwa katika imani yao na kutumwa kufanya huduma. Makanisa ya mtaa basi ni muhimu sana. Kwa ajili ya kurahisisha usimamizi; makanisa ya mtaa yamewekwa pamoja katika wilaya na majimbo.

KANUNI ZA IMANII

1. MUNGU WA UTATU

Tunamwamini Mungu mmoja aishiye milele, Mungu asiye na kikomo, Mwenye enzi na kiongozi-msimamizi wa ulimwengu; na kwamba Yeye pekee ndiye Mungu, muumbaji na kiongozi-msimamizi, mtakatifu kwa asili, sifa na tabia na kwa kusudi; na kwamba Yeye, kama Mungu, ni Mungu wa Utatu katika hali yake, anayedhihirika kama Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

(Mwanzo 1; Mambo ya Walawi 19:2; Kumbukumbu la Torati 6:4-5; Isaya 5:16; 6:1-7 40:18-31; Mathayo 3:16-17; 28:19-20; Yohana 14:6-27; 1 Wakorintho 8:6; 2 Wakorintho 13:14, Wagalatia 4:4-6; Waefeso 2:13-18)

2. YESU KRISTO

Tunamwamini Yesu Kristo, Nafsi ya Pili katika Utatu Uungu; na kwamba Yeye amekuwa daima mmoja na Baba; na kwamba alichukua asili na mwili wa mwanadamu na akazaliwa na Bikira Mariamu. Yesu si mwanadamu ambaye alikuwa Mungu, wala yeye si Mungu aliyevalia asili ya mwanadamu. Badala yake yeye ni Mungu kamili na mwanadamu kamili akiwa na nafsi mbili zilizounganishwa ziwe nafsi moja.

Tunaamini kwamba Yesu Kristo aliishi maisha yasio na dhambi ya utiifu mkamilifu, alikufa kifo cha dhabihu na kwa kufanya hivyo alishinda nguvu zote za uovu. Kupitia kwa nguvu za Mungu kuu, alifufuliwa kwa maisha na kama Mwana wa Mungu/Mwana wa Adamu mkamilifu alipaa mbinguni ambapo anatuombea.

(Mathayo 1:20-25; 16:15-16; Luka 1:26-35; Yohana 1:1-18; Matendo ya Mitume 2:22-36; Warumi 8:3, 32-34; Wagalatia 4:4-5; Wafilipi 2:5-11; Wakolosai 1:12-22; 1 Timotheo 6:14-16; Waebrania 1:1-5; 7:22-28; 9:24-28; 1 Yohana 1:1-3; 4:2-3,15)

3. ROHO MTAKATIFU

Tunamwamini Roho Mtakatifu, Nafsi ya tatu katika Utatu wa Uungu, ambaye anaushawishi ulimwengu kuhusu dhambi, na kuhuisha uzima wa kiroho katika wale wanaotubu na kuamini katika Yesu, anayeongoza, anafundisha na kuwatakasa waumini.

(Yohana 7:39; 14:15-18, 26; 16:7-15; Matendo ya Mitume 2:33; 15; 8-9; Warumi 8:1-27; Wagalatia 3:1-14; 4:6; Waefeso 3:14-21; 1 Wathesalonike 4:7-8:2 Wathesalonike 2:13; 1 Petro 1:2; 1 Yohana 3:24; 4:13)

4. MAANDIKO MATAKATIFU

Tunamini kwamba vitabu 66 vya Biblia ni neno la Mungu lililo na pumzi. Tunaamini kwamba Biblia inatuonyesha yote inayotupasa ili kujua wokovu wetu

(Luka 24:44-47; Yohana 10:35; 1 Wakorintho 15:3-4; 2 Timotheo 3:15-17; 1 Petro 1:10-12; 2Petro 1:20-21)

5. DHAMBI YA ASILI NA BINAFSI

Tunaamini kwamba dhambi iliingia ulimwenguni kupitia kwa kutotii kwa wazazi wetu wa kwanza, Adamu na Hawa. Dhambi hii ilileta kifo na kututenganisha kutoka kwa Mungu. Tunaamini kwamba kuna aina mbili za dhambi; dhambi ya asili au upotovu inayompinga Mungu, na dhambi anayotenda mtu binafsi.

5.1. Tunaamini kwamba kwa sababu ya dhambi ya Adamu, watu wote wanazaliwa na asili ya dhambi. Asili ya dhambi humpinga Mungu na kuendelea kuwavuta watu katika tendo la dhambi. Tunaamini kwamba asili ya dhambi inabaki ndani ya moyo wa Mkristo hadi wakati itakapotolewa kupitia kwa kazi za Roho Mtakatifu.

5.2. Dhambi ya asili ni tofauti na dhambi anayotenda mtu binafsi kwa sababu hii ni tamaa ya ndani ambayo inawaelekeza kutenda dhambi. Hakuna mtu anayewajibika kwa ajili ya dhambi ya asili hadi wakati wanakana au kupinga suluhisho la Mungu kwa ajili yake.

5.3. Dhambi ni tendo la makusudi la kuvunja amri ya Mungu. Si sawa na makosa, kusahau au upungufu, ambao ni matokeo ya hali ya mwanadamu iliyoanguka. Nia na majibu ambayo yako kinyume na Roho wa Kristo inaitwa dhambi za roho. Hakika dhambi ni uvunjaji wa sheria ya upendo, na kutoamini katika kazi ya Yesu ya wokovu.

(Dhambi ya Asili: Mwanzo 3:1-24; 6:5; Ayubu 15:14; Zaburi 51:5; Yeremia 17:9-10; Marko 7:21-23; Warumi 1:18-25; 5:12-14; 7:1-8:9; 1 Wakorintho 3:1-4; Wagalatia 5:16-25; 1 Yohana 1:7-8)

(Dhambi ya Binafsi: Mathayo 22:36-40 (pamoja na 1 Yohana 3:4) Yohana 8:34-36; 16:8-9; 1 Warumi 3:23; 6:15-23 8:18-24; 14:23; 1 Yohana 1:9-2:4; 3:7-10)

6. UPATANISHO

Tunaamini kwamba Yesu Kristo aliteseka, akamwaga damu na akafa msalabani ili kufanya upatanisho kamili na uliojaa wa dhambi na kuturudisha katika uhusiano na Mungu. Tunaamini kwamba hakuna njia nyingine ya kuokoka, na kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya watu **wote**. Yesu anapeana wokovu kwa watoto wadogo na wale wasioweza kufanya uamuzi wao wenyewe. Wengine **wote** ni lazima watubu na kuamini ili kupokea wokovu.

(Isaya 53:5-6, 11; Marko 10:45; Luka 24:46-48; Yohana 1:29; 3:14-17; Matendo ya Mitume 4:10-12; Warumi 3:21-26; 4:17-25 5:6-21; 1 Wakorintho 6:20; 2 2:19- 2Wakorintho 5:14-21; Wagalatia 1:3-4; 3:13-14; Wakolosai 1:19-23; 1 Timotheo 2:3-6; Tito 2:11-14, Waebrania 2:9; 11-14; 13:12: Petro 1:18-21; Yohana 2:1-2)

7. KUTENDA KWA HIARI

Tunaamini kwamba watu waliumbwa kwa mfano wa Mungu na kwa hivyo wana uwezo wa kuchagua kati ya mema na mabaya. Adamu alitenda dhambi na kwa sababu ya hiyo watu wote wanazaliwa na hali ya dhambi, na hawawezi kujiokoa kwa matendo yao mema.

Tunaamini kwamba neema Mungu ni ya bura na inapewa watu wote. Neema ya Mungu inawezesha mtu yeyote kubadili kutoka kwa dhambi hadi kwenye haki, na kumwamini Yesu kwamba anasamehe kuosha kutoka kwa dhambi kama watakubali.

Tunaamini kwamba hata kama mtu ameokoka na kuoshwa wanaweza kuanguka katika dhambi na kupotea milele wasipotubu kutoka kwa dhambi zao.

(Uungu na kuwajibika kimaadili: Mwanzo 1:26-27; 2:16-17; Kumbukumbu la Torati 28:1-2; 30:19; Yoshua 24:15; Zaburi 8:3-5; Isaya 1:8-10; Yeremia 31:29-30; Ezekieli 18:1-4; Mika 6:8; Warumi 1:19-20; 2:1-16; 14:7-12; Wagalatia 6:7-8)

(Kutoweza kwa kiasili: Ayubu 14:4; 15:14, Zaburi 14:1-4; 51:5; Yohana 3:6a; Warumi 3:10-12; 5:12-14, 20A; 7:14-25)

(Neema ya bure na matendo ya imani: Ezekieli 18:25-26; Yohana 1:12-13; 3:6b; Matendo 5:31; Warumi 5:6-8; 6:15- 16, 23; 10:6-8; 11:22; 1 Wakorintho 2:9-14; 10:1-12; 13; 2 Wakorintho 5:18-19; Wagalatia 5:6; Waefeso 2:8-10; Waefeso 2:8-10; Wafilipi 2:12-13, Wakolosai 1:21-23; 2 Timotheo 4:10a; Tito 2:11-14; Waebrania 2:1-3; 3:12-15; 6:4-6; 10:26-31; Yakobo 2:18-22; 2 Petro 1:10-11; 2:20-22)

8. TOBA

Tunaamini kwamba wote wametenda dhambi na wako mbali. Tunaamini Roho Mtakatifu anafanya kazi katika maisha ya watuu wote waliotenda dhambi na kuwarudisha kwa Mungu. Tunaamini kwamba wale wote wanaogeuka kutoka kwa dhambi kwa uaminifu wanatubu, na kuamini katika Kristo watapokea msamaha na maisha ya kiroho.

(2 Mambo ya Nyakati 7:14; Zaburi 32:5-6; 51:1-17; Isaya 55:6-7; Yeremia 3:12-14; Ezekieli 18:30-32; 33:14-16; Marko 1:14-15; Luka 3:1-14; 13:1-5; 18:9-14; Matendo ya Mitume 2:38; 3:19; 5:31; 17:30-31; 26:16-18; Warumi 2:4; 2 Wakorintho 7:8-11; 1 Wathesalonike 1:9; 2 Petro 3:9)

9. KUHESABIWA HAKI, KUHUISHWA, NA KUPOKELEWA

Tunaamini kwamba wale wote wanaomwamini Yesu Kristo na kumkubali kama Bwana na Mwokozi wamehesabiwa haki. Hii inamaanishwa kwamba Mungu husamehe dhambi zilizotendwa, anaweka huru kutoka kwa adhabu ya dhambi na kuwakubali kama haki.

10. Wakati mtu anamkubali Yesu kama Mwokozi, mtu huyo amezaliwa mara ya pili, na anapokea asili mpya ya maadili. Maisha haya mapya ya kiroho ni imani moja, upendo na utiifu kwa Mungu

11. Tunaamini kwamba Mungu katika neema yake hatusamehe tu, na kutupa maisha mapya ya kiroho, lakini anatupokea pia katika familia ya Mungu.

12. Mambo haya matatu, msamaha, kuzaliwa upya na kupokelewa, yote kutendeka kwa wakati mmoja na yanatanguliwa na toba na imani katika Kristo. Roho Mtakatifu anashuhudia kwa roho yetu na kutupa thibitisho kwamba Mungu ametuokoa.

(Luka 18:14; Yohana 1:12-13; 3:3-8; 5:24; Matendo ya Mitume 13:39; Warumi 1:17; 3:21-26, 28; 4:5-9, 17-25; 5:1, 16-19; 6:4; 7:6; 8: 1,15-17; 1 Wakorintho 1:30; 6:11; 2 Wakorintho 5:17-21; Wagalatia 2:16-21; 3:1-14,26; 4:4-7; Waefeso 1:6-7-2:1,4-5; Wafilipi 3:3-9; Wakolosai 2:13,Tito 3:4-7; 1 Petro 1:23; 1 Yohana 1:9; 3:1-2, 9; 4:7; 5:1, 9-13, 18)

10. UTAKASO WA KIKRISTO NA UTAKASO TIMILIFU

13. Tunaamini kwamba baada ya kuzaliwa mara ya pili, kuna kazi ingine ya Mungu ambayo waumini wote hujitoa kamili kwa Mungu, na wanawekwa huru kutokana na dhambi ya asili. Hii inawawezesha kuishi maisha ya upendo mtiifu kwa Mungu na kuwapenda wengine.

Wakati tumetakaswa, damu ya Yesu inatuosha mioyo yetu, na Roho Mtakatifu hutujaza mioyo yetu, akitupa nguvu za kumtumikia Mungu na kuishi maisha ya uungu. Roho Mtakatifu anashuhudia roho zetu ambazo ameosha na kutujaza.

Utakaso unawezekana kupitia kwa kifo cha Yesu. Upande wa utakaso wa mwanadamu unahusisha kuwekwa wakfu timilifu na imani kwamba Mungu atakutakasa. Ujuzi huu pia unajulikana kama “upendo mkamilifu,” “usafi wa moyo,” “ubatizo wa Roho Mtakatifu” na “utakatifu wa Kikristo.”

Tunaamini kwamba kuna tofauti kubwa kati ya moyo safi na tabia iliyokomaa. Mungu anaweza kutusafisha mioyo yetu katika tabia ya papo hapo inayopatikana kupitia ukuaji wa kiroho kwa muda mrefu.

Tunaamini kwamba mtu aliyetakaswa anayo tamaa ya kuku katika neema. Ukuaji huu si wa kujiendesha wenyewe, lakini ni lazima ulindwe kwa makini kupitia kwa nidhamu ya kiroho, ili kukuza tabia na utu wa mfano wa Kristo. Mtu ambaye hushughulikii kuku kiroho ataharibu ushahidi wao na neema ya Mungu katika maisha yao inaweza kusumbuka na ha ta kupotea.

(Yeremia 31:31-34; Ezekieli 36:25-27; Malaki 3:2-3; Mathayo 3:11-12; Luka 3:16-17; Yohana 7:37-39; 14:15-23; 17:6-20; Matendo ya Mitume 1:5; 2:1-4; 15:8-9; Warumi 6:11-13,19 8:1-4, 8-14; 12:1-2; 2Wakorintho 6:14-7:1; Wagalatia 2:20, 5:16-25; Waefeso 3:14-21, 5:17-18, 25-27; Wafilipi 3:10-15; Wakolosai 3:1-17; 1 Wathesalonike 5:23-24; Waebrania 4:9-11, 10:10-17, 12:1-2, 13:12; 1 Yohana 1:7, 9)

(“Ukamilifu wa Kikristo” na “Pendo kamilifu”. Kumbukumbu la Torati 30:6; Mathayo 5:43-48, 22:37-40; Warumi 12:9-21;, 13:8-10; 1 Wakorintho 13; Wafilipi 3:10-15 Waebrania 6:1; 1 Yohana 4:17-18)

(“Usafi wa Moyo”: Mathayo 5:8; Matendo ya Mitume 15:8-9; 1 Petro 1:22; 1 Yohana 3:3)

(“Ubatizo wa Roho Mtakatifu”: Yeremia 31:31-34; Ezekieli 36:25-27; Malaki 3:2-3; Mathayo 3:11-12; Luka 3:16-17; Matendo ya Mitume 1:5,2:1-4, 15:8-9)

(“Utimilifu wa Baraka”: Warumi 15:29)

(“Utakatifu wa Mkristo”: Mathayo 5:1-7:29; Yohana 15:1-11; Warumi 12:1-5:3; 2 Wakorintho 7:1; Waefeso 4:17-5:20; Wafilipi 1:9-11; 3:12-

15; Wakolosai 2:20-3:17; Wathesalonike 3:13, 4:7-8, 5:23; 2 Timotheo 2:19-22; Waebrania 10:19-25, 12:14; 13:20-21; 1 Petro 1:5-16, 2 Petro 1:1-11, 3:18; Yuda 20-21)

11. KANISA

15. Kanisa limeumbwa na watu wote ambao wanakiri Yesu Kristo kuwa Bwana. Watu hawa wameingia katika uhusiano wa agano na Mungu kupitia kuzaliwa upya na wamekuwa sehemu ya Mwili wa Kristo. Kanisa linaeleza maisha yake katika ibada ya umoja, kuhubiri neno la Mungu, kuhusika katika sakramenti, kumtii Kristo na kuhimizana katika maisha ya Kikristo.

Kanisa linapaswa kuendeleza kazi ya Kristo ulimwenguni kupitia maisha matakatifu, uinjilisti, uanafunzi na huduma ya matendo. Haya yote yanafanyika kupitia nguvu za Roho Mtakatifu.

Kanisa linaishi kama mkutano wa mtaa na mwili wa kimataifa, na linaeleza maisha yake na ibada katika njia tofauti na katika tamaduni tofauti. Kanisa linahakikisha kwamba Mungu anawaita watu kwa huduma maalum na kuwahimiza kuendeleza huduma za uinjilisti na utumishi wa upendo. Kanisa linaishi chini ya sheria za Mungu linaposubiri kuja kwa furaha kwa Bwana Yesu Kristo.

(Kutoka 19:3;Yeremia 31:33; Mathayo 8:11, 10:7, 16:13-19, 24; 18:15-20; 28:19-20; Yohana 17:14-26,20:21-23; Matendo ya Mitume 1:7-8; 2:32-47; 6:1-2, 13:1, 14:23; Warumi 2:28-29, 4:16; 10:9-15; 11:13-32; 12:1-8; 15:1-3; 1 Wakorintho 3:5-9; 7:17; 11:1; 17-33; 12:3; 12:31; 14:26-40; 2 Wakorintho 5:11-6:1; Wagalatia 5:6; 13-14; 6:1-5, 15; Waefeso 4:1-17; 5:25-27;

Wafilipi 2:1-16; 1 Wathesalonike 4:1-12, 1 Timotheo 4:13, Waebrania 10:19-25; 1 Petro 1:1-2,13; 2:4-12, 21; 4:1-2, 10-11 1 Yohana 4:17; Yuda 24; Ufunuo 5:9-10)

12. UBATIZO

16. Tunaamini kwamba ubatizo wa Mkristo ni sakramenti iliyoamriwa na Yesu Kristo. Ubatizo hutangaza imani ya mtu katika kifo na ufufuo wa Yesu Kristo na tamaa ya kumfuata Yesu katika utiifu na haki.

Kwa kuwa ubatizo ni ishara ya Agano mpya, watoto wadogo wanaweza kubatizwa, kwa maombi ya wazazi au walezi wao ambao watatoa hakikisho la malezi ya Kikristo yanayohitajika kwa watoto wanaobatizwa.

Watu wanaweza kubatiza kutekelezwa kwa kuzamishwa ndani ya maji, kunyunyiziwa au kumwagiwa maji, kulingana na chaguo la anayebatizwa.

(Mathayo 3:1-7; 28:16-20; Mtendo ya Mitume 2:37-41; 8:35-39; 10:44-48; 16:29-34; 19:1-6; Warumi 6:3-4; Wagalatia 3:26-28; Wakolosai 2:12; 1 Petro 3:18-22)

13. MEZA YA BWANA

17. Tunaamini kwamba meza ya Bwana ilianzishwa na Yesu. Ni ukumbusho wa dhabihu ya Yesu na huleta maisha ya kiroho na baraka kwa wale wote wanaoipokea katika imani. Ni ya wale wote walio na imani katika Kristo, na kuamini kwamba kupitia kifo chake, wamepokea uhai na wokovu. Utumishi wa umoja pia unatukumbusha kwamba Yesu atarudi tena.

Ni wale walio na imani katika Kristo na wanawapenda waumini wenzao wanapaswa kushiriki katika ibada ya umoja.

(Kutoka 12:1-14; Mathayo 26:26-29; Marko 14:22-25; Luka 22:17-20; Yohana 6:28-58; 1 Wakorintho 10:14-21, 11:23-32)

14. UPONYAJI WA KIMUNGU

18. Tunaamini kwamba Mungu huwaponya wagonjwa kwa kujibu maombi yaya watu hawa na kuwatia watu moyo kuomba katika imani kwa uponyaji wa wagonjwa. Pia tunaamini Mungu huponya kupitia njia ya madawa ya kisayansi.

(2 Wafalme 5:1-19;Zaburi 103:1-5; Mathayo 4:23-24; 9:18-35; Yohana 4:46-54; Matendo 5:12-16; 9:32-42; 14:8-15; 1 Wakorintho 12:4-11; 2 Wakorintho 12:7-10; Yakobo 5:13-16)

15. KUJA KWA PILI KWA KRISTO

19. Tunaamini kwamba Bwana Yesu Kristo atarudi tena. Wale waumini wanaoishi hawataenda mbele ya wale waliolala tayari. Wale waliokaa ndani ya Yesu, watanyakuliwa na watakatifu waliofufuliwa kukutana na Bwana angani, ili tuwe na Bwana wakati wote.

(Mathayo 25:31-46; Yohana 14:1-3; Matendo ya Mitume 1:9-11; Wafilipi 3:20-21; 1 Wathesalonike 4:13-18; Tito 2:11-14; Waebrania 9:26-28; 2 Petro 3:3-15; Ufunuo 1:7-8; 22:7-20)

16. UFUFUO, HUKUMU, NA KIAMA

20. Tunaamini kwamba miili ya wenye haki na wasio wa haki itafufuliwa kutoka kwa wafu na kuunganishwa tena na roho zao.

21. Tunaamini kwamba kutakuwa na wakati wa hukumu ambapo kila mtu atasimama mbele ya Mungu ili ahukumiwe kulingana na mtendo yake wakati wa uhai huu.

22. Tunaamini kwamba wale wanaokataa kutubu na kuamini katika Kristo watateseka milele katika jehanam. Tunaamini pia kwamba maisha ya utukufu na uzima wa milele yamehakikishiwa wote ambao wanamwamini kwa wokovu, na kumfuata kwa utiifu, Yesu Kristo Bwana wetu.

(Mwanzo 18:25; 1 Samweli 2:10; Zaburi 50:6; Isaya 26:19; Daniel 12:2-3; Mathayo 25:31-46; Marko 9:43-48; Luka 16:19-31; 20:27-38; Yohana 3:16-18; 5:25-29; 11:21-27 Matendo 17:30-31; Warumi 2:1-16; 14:7-12; 1 Wakorintho 15:12-58; 2 Wakorintho 5:10; 2 Wathesalonike 1:5-10; Ufunuo 20:11-15; 22:1-15)

Sheria za Washirika wa Kanisa

Watu ambao wamempokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao, na wanapenda kujiunga katika ushirika wa Kanisa la Mnazareti lazima waishi maisha matakatifu yanayompendeza Mungu. Neno la Mungu linatueleza jinsi tunavyopaswa kuishi.

Mwanachama wa Kanisa anatakiwa kufanya yafuatayo (27.1)

1. Mpende Mungu kwa moyo wetu wote, nafsi yetu yote, nia yote, na kwa nguvu zote, na kumpenda jirani yako kama nafsi yako. (Kutoka 20:3-6, Mambo ya Walawi 19:17-18, Kumbukumbu la Torati 5:7-10,6:4-5 Marko 12:28-31, Warumi 13:8-10).

2. Kushiriki injili na wale ambao hawajaokoka, kuwakaribisha Kanisani, na kutafuta kuwaongoza kwa Kristo. (Mathayo 28:19-20 Matendo ya Mitume 1:8 Warumi 1:14-16, 2 Wakorintho 5:18-20)

3. Waheshimu watu wote (Waefeso 4:32, Tito 3:2, 1 Petro 2:17, 1 Yohana 3:18)

4. Kuwa msaada, mkarimu, mtulivu, kuwasamehe Wakristo wenzako. Warumi 12:13, Wagalatia 6:2,10, Wakolosai 3:12-14

5. Jitahidi kutenda mema kwa wote wenye njaa wagonjwa, waliofungwa na kuwahudumia wahitaji. kadiri ya nafasi na uwezo tunaopewa (Mathayo 25:35-36, 2 Wakorintho 9:8-10, Wagalatia 2:10, Yakobo 2:15-16, 1 Yohana 3:17-18)

6. Toa fungu la kumi na sadaka ili kutegemeza na kuendeleza kazi za kanisa (Malaki 3:8-10, Luka 6:38, 1 Wakorintho 9:14; 16:2, 2 Wakorintho 9:6-10, Wafilipi 4:15-19)

7. Hudhuria kwa uaminifu ibada za Kanisa. (Waebrania 10:25, Matendo ya Mitume 2:42) kushiriki sakramenti, (1 Wakorintho 11:23-30), kuwa na maombi binafsi, na kufanya ibada za nyumbani pamoja na familia (Matendo ya Mitume 17:11, 2 Timotheo 2:15, 3:14-16, Kumbukumbu la Torati 6:6-7, Mathayo 6:6)

B. Washirika wa Kanisa wanatakiwa wajiepushe na mambo yafuatayo (27.2):

1. Kulitaja bure jina la Bwana Mungu (Kutoka 20:7, Mambo ya Walawi 19:12, Yakobo 5:12)

2. Kutenda mambo yasiyohitajika Siku ya Bwana ili kwamba ipoteze maana yake ya utakatifu (Kutoka 20:8-11, Isaya 58:13-14, Marko 2:27-28, Mtd 20:7, Ufunuo 1:10)

3. Aina yo yote ya Uzinzi, (Kutoka 20:14, Mathayo 5:27-32 1 Wakorintho 6:9-11, Wagalatia 5:19, 1 Wathesalonike 4:3-7)

4. Tabia na mazoea ambayo ni ya uharibifu kwetu kimwili na akili. Tunapaswa kukumbuka kuwa sisi ni hekalu la Roho Mtakatifu (Mithali 20:1; 23:1-3, 1 Wakorintho 6:17-20, 2 Wakorintho 7:1, Waefeso 5:18)

5. Kugombana, kusengenya, kueneza **hadithi zinazoumiza majina ya watu wengine** uvumi unaochafua majina au sifa za watu wengine (2 Wakorintho 12:20, Wagalatia 5:15, Waefeso 4:30-32, Yakobo 3:5-18, 1 Petro 3:9-10)

6. Kutokuwa mwaminifu, danganyifu katika biashara, na kusema uwongo. (Mambo ya Walawi 19:10-11, Warumi 12:17, 1 Wakorintho 6:7-10).

7. Kiburi kwa ajili ya mavazi au tabia. Watu **wanapaswa kuvaa mavazi ya heshima ili kuonyesha maisha matakatifu** (Mithali 29:23, 1 Timotheo 2:8-10, Yakobo 4:6, 1 Petro 3:3-4, 1 Yohana 2:15-17).

8. **Muziki, vitabu, magazeti na starehe zisizoleta heshima kwa Mungu.** 1 Wakorintho 10:31, 2 Wakorintho 6:14-17, Yakobo 4:4

Huwa tunasema:

Kuwa na ushirika mwema na Kanisa. Bila kuwa kinyume na uongozi wa Kanisa bali kujitoa kikamilifu, kushika na kutekeleza mafundisho yake, na kujihusisha na kazi za Kanisa, kama vile ushuhuda na kuwafikia wengine kwa ajili ya Kristo. (Waefeso 2; 18-22, 4:1-8; 11-16; Wafilipi 2:1-8; 1 Petro 2:9-10)

Agano la Maadili ya Kikiristo

(Hii ni tafsiri fupi zaidi na iliyorahisishwa ya Agano la Maadili ya Kikristo. Unaweza kutazama katika Kitabu cha Mwongozo (Manual ukurasa wa 46-60) kwa maneno rasmi na maelezo yote)

A. Maisha ya Kikristo

33. Kanisa hutangaza kwa furaha habari njema kwamba tukombolewe kutoka kwa dhambi na kuwa na maisha mapya katika Kristo. Kwa neema ya Mungu, sisi Wakristo hatunapaswi tena kufuata asili ya dhambi na utu wa kale. Bali tunapaswa "kuvalia utu mpya" – mwenendo mpya na mtakatifu wa maisha pamoja na nia ya Kristo. [Waefeso 4:17-24]

33.1. Kanisa la Mnazareti linakusudia kueleza kanuni za Biblia kwa jamii ya kisasa kwa njia ambayo kanuni na sheria za kanisa zitajulikana na kueleweka katika utamaduni tofauti. Tunashikilia kwamba Amri Kumi, kama zina msingi wa elimu ya maadili ya Kikristo na tunapaswa kuzitii kwa kila hali.

33.2. Pia tunaamini kwamba Roho Mtakatifu huongoza kanisa kujenga dhamira ya Kikristo ya umoja. Kanisa la Mnazareti ni kanisa kama kanisa la kimataifa hutafuta njia za kuendeleza njia takatifu ya maisha. Agano la Maadili ya Kikiristo linapaswa kufuata kwa makini kama mwongozo na msaada wa kuishi kitakatifu. Watu wasiofuata mwongozo huu wanaumiza ushahidi wa kanisa kudhoofhisha maisha yao ya kiroho.

33.3. Haiwezekani, na wala haisaidii, kuorodhesha kila dhambi inayojulikana ulimwenguni. Ni muhimu kwamba washirika wa

kanisa watafute msaada wa Roho Mtakatifu ili kutofautisha kati ya mema na mabaya. “Jaribuni mambo yote. Lishikeni lililo jema. Jitengeni na ubaya wa kila namna.” (1 Wathesalonike 5:21-22)

33.4. Viongozi wa Kanisa wanapaswa kupeana mafundisho ya Kibiblia ambayo yatawasaidia watu kutenganisha kati ya mema na mabaya.

33.5. Elimu ni muhimu sana kwa ustawi au ufanisi wa kijamii na kiroho katika jamii. Shule za umma zina wajibu wa kuelimisha wote. Ni muhimu kwamba kanisa kupitia Shule za Jumapili, shule za kawaida, vituo vya malezi na seminari vifundishe kanuni za kibiblia na vipimo vya hali ya juu vya maadili. Mafundisho ya kitakatifu yanapaswa pia yatekelezwe katika nyumba zetu. Wakristo wanapaswa kutiwa moyo kufanya kazi katika shule za umma na kutoa ushuhuda wa Kikristo na ushawishi.

34. Mambo yafuatayo ni lazima yaepukwe:

34.1. Starehe ambazo ni haribifu kwa Maadili ya Kikristo. Wakristo wanatakiwa kufuata kanuni tatu muhimu.

1. Uwakili wa Kikristo kwa wakati wa starehe na pia wakati wa kazi.
2. Wakristo wameitwa kuishi maisha matakatifu. Kuna vitabu, vingi, redio na vipindi vya runinga na mambo kwenye mtandao ambayo yanaingia katika nyumba zetu. Ni lazima tujikinge na fasihi na vipindi ambavyo vitatutenganisha na Mungu na maisha matakatifu. Tunapaswa kuunga mkono na kuhimiza yale mambo ambayo ni mazuri na ya kusaidia.
3. Kama Wakristo ni wajibu wetu kupinga mambo yanayomkufuru Mungu na kuendeleza uovu, vita na uasherati. Tunapaswa kujiepusha na starehe zote zinazosababisha dhambi kuonekana ya kuvutua na kufurahisha, na kushusha vipimo vya Mungu vya utakatifu wa moyo na maisha.

Watu wetu wanapaswa kufundishwa kutumia utambuzi wa maombi wakati wote katika kuchagua njia kuu ya kuishi

kitakatifu. Tunapaswa kutumia kipimo kinachofuata ambacho kilichopewa na John Wesley, na mama yake, "Chochote kidhoofishacho kinachodhuru dhamira yako, kinachozuia hisia zako kwa Mungu, kiondoacho kuvutiwa kwako na mambo ya kiroho, cho chote kinachoongeza mamlaka ya mwili wako juu ya dhamiri yako, kitu hicho kwako ni dhambi". (Warumi 14:7-13; 1 Wakorintho 10:31-33, Waefeso 5:1-18, Wafilipi 4:8-9; 1 Petro 1:13-17; 2 Petro 1:3-11)

34.2. Jiepushe na bahati nasibu na aina nyingine za kamari kwa vile mambo haya yanadhuru mtu binafsi na jamii kwa jumla. (Mathayo 6:24-34; 2 Wathesalonike 3:6-13; 1 Timotheo 6:6-11; Waebrania 13:5-6; 1 Yohana 2:15-17)

34.3. Usiwe na ushirika na makundi yaliyofungamanishwa na siri za kiapo. (1 Wakorintho 1:26-31, 2 Wakorintho 6:14-7:1; Waefeso 5:11-16; Yakobo 4:4, 1 Yohana 2:15-17)

34.4. Jiepushe na aina zote za dansi na ngoma ambazo zinazuia ukuaji wa kiroho na kuvunjika kwa tabia ya uadilifu na staha inayopaswa kudumishwa. (Mathayo 22:36-39, Warumi 12:1-2, 1 Wakorintho 10:31-33, Wafilipi 1:9-11, Wakolosai 3:1-17)

34.5. Jiepushe na matumizi ya pombe au aina yo yote ya kileo. Kuuza au kutumia tumbako au madawa ya kulevya kama vile marijuana.

Biblia pamoja na ujuzi wa kibinadamu huthibitisha kuwa kunywa vinywaji vya pombe na matumizi ya tumbaku inaweza kusababisha matatizo mengi ya kijamii. Kwa vile lengo letu ni kuishi maisha matakatifu basi tunapaswa kuacha kutumia vitu hivi. Biblia inafundisha kwamba miili yetu ni hekalu la Roho Mtakatifu, kwa hivyo Maisha yetu yanapaswa kuwa ushahidi mwema kwa wengine.

(Mithali 20:1; 23:29-24:2; Hosea 4:10-11; Habakuki 2:5; Warumi 13:8; 14:15-21; 15:1-2; 1 Wakorintho 3:16-17; 6:9-12, 19-20; 10:31-33; Wagalatia 5:13-14, Waefeso 5:18)

34.6. Tunakataza matumizi ya dawa za nguvu zinazoathiri kufikiria au hisia za mtu, bila usimamizi halisi wa daktari. (Mathayo 22:37-39, 27:34, Warumi 12:1-2, 1 Wakorintho 6:19-20; 9:24-27)

B. Ndoa na Talaka

35. Kuna nguvu nyingi zinazofanya kazi katika jamii kudhoofisha na kuharibu ndoa na familia za Kikristo. Ni muhimu kwamba wachungaji wahubiri wazi mpango wa kibiblia ya kwamba ndoa inapaswa kuwa ya kudumu. Makanisa yanahitajika kuanzisha vipindi ambavyo vitatia nguvu na kusaidia familia za Kikristo.

Ndoa iliamriwa na Mungu ni muungano wa kirafiki wa mwanaume mmoja na mwanamke mmoja kwa ajili ya ushirika, usaidizi, na kuzaa kwa watoto. Watu wetu hawapaswi kuingia ndani ya ndoa kwa haraka bali baada ya maombi kwa uongozi wa Mungu. Agano la ndoa la kufunganisha mradi tu wanapoishi, na kuvunja ndoa ni uharibifu wa mpango wa Mungu wa kudumu kwa ndoa. (Mwanzo 1:26-28, 31; 2:21-24; Malaki 2:13-16; Mathayo 19:3-9 Yohana 2:1-11; Waefeso 5:21-6:4; 1 Wathesalonike 4:3-8; Waebrania 13:4)

35.1. Biblia inafundisha kwamba ndoa ni kujitoa kwa mwanamume na mwanamke mmoja kwa mwenzake wakati wote wa maisha yao, wakidhiirisha mfano wa upendo wa dhabihu wa Kristo kwa kanisa. Ndoa imekusudiwa kuwa ya kudumu na talaka ni kuvunja au kukaidi mafundisho dhairi ya Kristo. Takala yaweza kusamehewa kwa neema ya Mungu ikiwa neema hiyo itatafutwa katika hali ya toba, imani na unyenyekevu. Tunatambua kwamba watu wengine wanalazimishwa kupewa talaka kinyume na matakwa yao, au hulazimishwa kutaliki ili kujiepusha na mafarakano au kupata ulinzi wa kisheria.

(Mwanzo 2:1-24; Marko 10:2-12; Luka 7:36-50; 16:18; Yohana 7:53-8:11; 1 Wakorintho 6:9-11; 7:10-16; Waefeso 5:25-33)

35.2. Wahudumu wa Kanisa la Mnazareti wanapaswa kufundisha waumini wao utakatifu wa ndoa. Wanapaswa kupeana ushauri kwa wanaooana kabla ya kutekeleza arusi. Hii inawahusu pia wale kutalikiwa na wangependa kuoa tena. Wahudumu

watatekeleza arusi kwa wale walio na ufahamu wa kibiblia wa ndoa.

35.3. Washirika wa Kanisa walio katika ndoa zisizokuwa na furaha wanapaswa kutafuta njia ya kusuluhisha matatizo hayo. Hii inapaswa kufanywa kwa amani kulingana na viapo vyao na mafundisho dhahiri ya Maandiko. Wanapaswa kutafuta kulinda familia zao na wala wasisababishe aibu kwa Kristo au Kanisa lake. Mume na mke wanaokabiliwa na tatizo mbaya la ndoa, wanapaswa kutafuta mawaidha au mashauri ya mchungaji wao na viongozi wengine wanaofaa wa kiroho.

35.4. Kwa sababu ya kutokujua, dhambi na udhaifu wa kibinadamu, watu wengi hafuati mpango wa Mungu. Tunaamini kwamba Kristo anaweza kuwakomboa watu hao kama vile alivyomkomboa yule mwanamke Msamaria. Mahali ambapo watu wametalikiwa na wakaoa tena, wanapaswa kutafuta neema ya Mungu na msaada wake katika uhusiano wa ndoa yao. Watu kama hao wanaweza kukubaliwa kuwa washirika wa kanisa baada ya kudhihirisha ushahidi wa kutubu na kuzaliwa upya kwao na ufahamu wao wa utakatifu wa ndoa ya Kikristo.

C. Kusababisha Utoaji Mimba

36. Kanisa la Mnazareti linaamini kwamba uhai, hata ule wa mtoto ambaye hajazaliwa ni wa utakatifu na tumepewa na Mungu. Tunapinga utoaji wa mimba kwa njia yo yote. Tunatambua kwamba kuna sababu chache ambapo maisha ya mama, au mtoto ambaye hajazaliwa, au wote wamo katika hatari. Katika hali kama hizo, utoaji wa mimba unapaswa kufanyika tu baada ya kupata ushauri unaofaa wa kimatibabu na Kikristo.

Tunapinga utoaji wa mimba na kwa hivyo ni lazima pia tujitoe kwa kuanzisha na kusaidia miradi ambayo itatoa misaada kwa kina mama na watoto. Mahali ambapo kuna tatizo la mimba isiyotakikana, kanisa linahitaji kutoa msaada wa upendo, maombi na ushauri. Hii inaweza kuhusisha nyumba za mama wajaa wazito na kuanzishwa kwa huduma za Kikristo za kulea.

Mara nyingi watu hutafuta utoaji wa mimba kwa sababu hajafuata viwango vya Kikristo vya jukumu la mapenzi. Kanisa linahitajika kutoa mafundisho dhahiri juu ya hali ya kimapenzi ya mwanadamu kulingana na misingi ya Kikristo.

(Mwanzo 2:7, 9:6; Kutoka 20:13; 21:12-16; Mambo ya Walawi 18:21; Ayubu 31:15; Zaburi 22:9; 139:3-16; Isaaya 44:2, 24; 49:5; Yeremia 1:5; Luka 1:23-25; 36-45, Matendo ya Mitume 17:25; Warumi 12:1-2; 1 Wakorintho 6:16; 7:1ff; 1 Wathesolonike 4:3-6)

D. Maumbile ya Kiume na Kike

37. Maumbile ya kiume na kike ni dhihirisho la utakatifu na uzuri ambao Mungu alikusudia kwa viumbe vyake. Ni mojawapo ya njia ambazo agano kati ya mume na mke linatiwa muhuri na kudhihirishwa. Maumbile ya kiume na kike yametakaswa na Mungu wakati yanapatikana ndani ya ndoa na upendo na uaminifu.

Watoto wanapaswa kufundishwa tabia ya utakatifu ya maumbile ya kiume na kike kulingana na muktadha wa upendo, uvumilivu, na uaminifu nyumbani kwa Wakristo.

Wahudumu na walimu wanapaswa kueleza wazi ufahamu wa Kikristo kuhusu hisia za mapenzi katika maumbile ya mwanadamu. Wanapaswa kuwasisitizia Wakristo kuona uzuri na utakatifu wake na kulinda kwa bidii kusalitiwa na kupotoshwa kwa maana yake.

Aina zote za uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa kati ya mwanamume na mwanamke ni kinyume na sheria za Mungu.

Ulawiti ni njia moja ambayo hisia za mapenzi zinapotoshwa na watu wengine. Tunatambua msimamo wa Biblia kwamba vitendo kama hivyo ni dhambi na huleta ghadhabu ya Mungu. Tunaamini kwamba neema ya Mungu inatosha kumaliza mazoea ya ulawiti (1 Wakorintho 6:9-11). (Mwanzo 1:27; 19:1-25; Mambo ya Walawi 20:13; Warumi 1:26-27; 1 Wakorintho 6:9-11; 1 Timotheo 1:8-10)

E. Uwakili wa Kikristo

38. Maana ya Uwakili. Maandiko yanafundisha kwamba Mungu ndiye anayemiliki watu wote na vitu vyote. Sisi ni mawakili wa kulinda na kutumia vyema uhai na mali tuliyo nayo.

Siku moja tutatoa hesabu ya uwakili wao mbele ya Mungu. Mungu ameweka utaratibu wa kutoa zaka ambayo inamaanisha kumtolea Mungu sehemu ya kumi ya mapato yetu. Hii inaonyesha kumiliki kwa Mungu na uwakili wetu.

(Malaki 3:8-12; Mathayo 6:24-34; 25:31-46; Marko 10:17-31; Luka 12:13-24; 19:11-27; Yohana 15:1-17; Warumi 12:1-13; 1 Wakorintho 9:7-14; 2 Wakorintho 8:1-15; 9:6-15; 1 Timotheo 6:6-19; Waebrania 7:8; Yakobo 1:27; 1 Yohana 3:16-18)

38.1. Kuleta Zaka Ghalani. Kuleta zaka ghalani ni tendo la Maandiko na njia ya Kimatendo ya washirika wa kanisa kutoa zaka zao kwa uaminifu na kila mara kwa kanisa lao la mtaa. Washirika wote wa Kanisa la Mnazareti wanaombwa kutoa kwa uaminifu aghalau sehemu ya kumi ya mapatao yao kwa kanisa lao la mtaa. Sadaka ya hiari inapaswa kutolewa kwa kuongezea, ili kusaidia kanisa lote la mtaa, wilaya, jimbo, na viwango vya Vikuu.

Makanisa ya mtaa yanaombwa kulipa bajeti ya wilaya, jimbo, na ya inayotolewa kila mwezi.

38.3. Kutegemeza Huduma. “Vivyo hivyo Bwana ameamuru kwamba wale wanaohubiri injili wapate riziki zao kwa hiyo injili” (1 Wakorintho 9:14). Kanisa lina wajibu wa kutegemeza au kusaidia wahudumu wake ambao wameitwa na Mungu, na ambao wamejitoa kikamilifu kwa kazi ya huduma. Ili kutekeleza haya washirika wa kanisa wanapaswa kutoa kutoa zaka zao kila wakati na kulipa mchungaji wao kila juma.

38.4. Urithi na Zawadi za Mapato. Wakristo wanapaswa kuwa waaminifu katika kulipa zaka na kutoa sadaka wakati wako hai. Wanapaswa kufikiria pia ni nini watafanya na fedha na mali ambayo wameachwa nayo kabla hawajafa. Wakristo wanapaswa kufanya wosia na kufikiria kutoa kwa kazi ya kanisa inayoendelea.

F. Viongozi wa Kanisa

39. Tunaagiza makanisa yetu ya mtaa kuchagua kama viongozi wa kanisa watu ambao wanadhihirisha wazi ujuzi wa utakaso kamili na wanaodhihirisha maisha matakatifu kupitia kwa neema ya Mungu.

Wanapaswa pia kukubaliana na mafundisho, uongozi na utaratibu wa Kanisa la Mnazareti na ambao wanasaidia na kutegemeza kanisa la mtaa kwa maudhurio, zaka na sadaka kwa uaminifu.

G. Kanuni za Utengamano

40. Kanisa linapaswa kufuata utaratibu kulingana na sheria ya *Robert's Rules of Order* katika kuendesha shughuli za mikutano ya kanisa katika mtaa, wilaya, jimbo na kanisa kuu.

H. Kurekebisha Agano la Maadili ya Kikristo

41. Agano la Maadili ya Kikristo inaweza kubadilishwa au kurekebishwa ikiwa jambo hilo litakubaliwa kwa theluthi mbili za kura za wajumbe wote katika mkutano wa kikao kikuu.

UONGOZI KATIKA KANISA

Kuna njia kuu tatu za kuweka uongozi katika Kanisa

1. Makanisa mengine yanayo viongozi walio na madaraka nyingi.
2. Makanisa mengine huwapa washirika madaraka makubwa sana. Hakuna kiongozi au mtu mmoja mwenye madaraka makubwa sana badala yake viongozi hushirikiana na makasisi wa Kanisa.
3. Utawala wa uwakilishi ambapo mamlaka yanashirikishwa na wahudumu na kongamano lote.

Kanisa la Mnazareti lina utawala wa uwakilishi na lina mchungaji na kamati ya kanisa ambayo wanashirikiana katika majukumu ya kuongoza na kutawala kazi za Kanisa.

Tunaamini kuwa ni muhimu kuwa na msimamizi anayesaidia kusimamia makanisa ya mtaa katika kutimiza utume na malengo. Mamlaka ya msimamizi yasiingilie uhuru katika hatua zinazochukuliwa na Kanisa lililoratibiwa. Kila Kanisa la mtaa lifurahie uhuru wa kuchagua mchunguji wake litunze na kuangalia shughuli za fedha na mambo yote yanayohusiana na maisha na kazi ya Kanisa la mtaa. **(28-28.2)**

MUUNDO WA UTAWALA KATIKA KANISA LA MNAZARETI

Dr Bresee ambaye ni muasisi (aliyeanzisha) wa Kanisa la Mnazareti alikuwa mtumishi katika Kanisa la Kimethodist kwa miaka nyingi. Aliona kuwa Kanisa lilihitaji viongozi wa kuwatia moyo na kuwasimamia wachungaji. Hakutumia neno Askofu lakini aliwaita viongozi hao kama wasimamizi. Kwa hiyo unaweza kuona kuwa waangalizi ni kama timu ya viongozi wanaofundisha, kuwatia moyo na kuwajenga wachungaji katika wilaya.

Katika sehemu ya mashariki ya Amerika (USA); kulikuwa na makanisa mengine yaliyokuwa yakihubiri kwa nguvu sana kuwa Wakristo wanahitaji kuisha maisha ya utakatifu. Makanisa hayo yalihisi wakati mwingine maaskofu waliingilia sana na shughuli za makanisa ya mtaa. Kwa hiyo yaliona hitaji la halmashauri za Kanisa kuwa na mamlaka katika kusimamia uendeshaji shughuli za Kanisa la mtaa.

Wakati makundi hayo mawili yalipoamua kuwa pamoja na kuanzisha Kanisa la Mnazareti walifanya kazi kwa bidii sana kutafuta njia ya kuunganisha tofauti hizi juu ya uongozi. Walikubaliana kuwa walihitaji waangalizi ambao wangewatia moyo na kutoa ushauri kwa uongozi wa makanisa. Pia walikubaliana kuwa makanisa ya mtaa yawe na mamlaka ya kuchagua wachungaji wanaowataka na waweze kuangalia mambo ya kila siku ya utendaji, wafanye kazi kwa pamoja na kamati ya Halmashauri ya Kanisa katika utendaji wa shughuli za Kanisa.

Katika ngazi ya wilaya, Msimamizi wa wilaya anafanya kazi pamoja na Halmashauri ya wilaya (DAB) katika kuyaelekeza makanisa. Katika ngazi ya kimataifa wasimamizi wakuu wanafanya kazi kwa pamoja na Halmashauri ya Wazimamizi Wakuu.

Kuna ngazi tatu katika utawala wa Kanisa la Mnazareti ambazo ni:

- Kanisa la Mtaa
- Mkutano wa Wilaya
- Mkutano Mkuu (kikao kikuu)

Ni muhimu kuelewa jinsi kila ngazi inavyofanya kazi na hivyo kuelewa jinsi Kanisa zima linavyofanya kazi.

KANISA LA MTAA

Sehemu muhimu sana katika Kanisa la Mnazareti ni Kanisa la mtaa. Hapa ndipo watu wanakuja kuabudu, watu wasiokuwa Wakristo wanafanywa Wakristo na kukua katika maisha ya Ukristo. Hapa ndipo mahali watu wanakuwa washirika wa Kanisa.

USHIRIKA WA KANISA (107-110)

Kuna mambo manne ambayo mtu lazima afanye ili apokelewe kuwa mshirika wa Kanisa la Mnazareti:

1. Ashuhudie kuwa amempokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi.
2. Awe amekubaliana na kanuni za imani za Kanisa la Mnazareti.
3. Aahidi kufuata sheria za washirika za Kanisa la Mnazareti.
4. Aahidi kusaidia Kanisa kwa kutumia muda wake, kipaji na mali yake na kwa uaminifu kabisa kushughulikia mipango yote ya Kanisa na kulisaidia Kanisa kifedha.

Mshirika wa Kanisa ni zaidi ya mtu anayehudhuria Kanisani. Mshirika wa Kanisa ni mtu ambaye amejitoa hadharani na yuko mstari wa mbele katika kuhakikisha Kanisa la mtaa linasimama.

Anahakikisha Kanisa la mtaa linafanikiwa malengo yake ya utume.

JINSI YA KUWA MSHIRIKA

1. Watu wanaotaka kuwa washirika lazima wajue kuwa Yesu ni Mwokozi wao
2. Ni lazima wahudhurie madarasa yanayoeleza mafundisho muhimu ya Kanisa
3. Ni lazima wahudhurie madarasa yanayoeleza sheria za Kanisa za jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo

Kamati ya Uinjilisti na Kamati ya washirika na Kanisa liwahoji watu wanaopenda kuwa wanachama. Kama wakipitishwa, basi watapokelewa katika uanachama wa Kanisa na mchungaji katika ibada ya hadhara Kanisani.

MIKUTANO YA KANISA (113)

Mkutano wa Kanisa ni mkutano rasmi wa Kanisa la mtaa ambapo washirika wa Kanisa hukutana pamoja kuzungumza na kufanya maamuzi kuhusu uhai, kukua na uongozi wa Kanisa la mtaa.

- Mchungaji ni mwenyekiti
- Katibu wa halmashauri ya Kanisa ndiye atakuwa mwandishi wa mkutano wa kanisa.
- Mkutano Mkuu wa Mwaka lazima ufanyike miezi mitatu Kabla ya mkutano mkuu wa wilaya

Idadi ya makanisa inayoongezeka ina vikundi vya akina mama na vikundi vya akina baba kama sehemu na mipangilio ya shughuli za Kanisa. Mambo haya hayapo katika manual lakini makanisa mengi ya Manazareti yanayapa umuhimu makundi hayo.

Kazi ya Mkutano Mkuu wa Kanisa

Mkutano huu una kazi mbili

1. Kupokea ripoti
2. Kufanya uchaguzi

Mkutano wa Kanisa utapokea Ripoti Kutoka kwa

1. Mchungaji (413.5)
2. Rais wa NMI (153.2)
3. Rais wa NYI (151.3)
4. Rais wa Kikundi cha akina mama
5. Kikundi cha akina baba
6. Wale walio na leseni za uchungaji za mtaa (428.1)
7. Katibu wa hamshauri ya kanisa (135.2)
8. Mtunza hazina (136.5)
9. Msimamizi wa Shule ya Jumapili (146.6)

Mkutano mkuu wa mwaka lazima ufanye uchaguzi wa wafuatao:-

1. Mawakili (137)
2. Wadhamini (141, 142.1)
3. Msimamizi wa Shule ya Jumapili (146)
4. Halmashauri ya Huduma ya Shule ya Jumapili (145)
5. Mwenyekiti wa akina mama
6. Mwenyekiti wa akina baba

Kazi ya Mchungaji

Mchungaji ni kasisi au mhudumu ambaye ana cheti cha uchungaji cha wilaya. Mchungaji lazima awe ana wito wa Mungu kuhubiri neno la Mungu na kuwachunga watu wa Mungu. Mchungaji ana kazi nyingi ya kufanya. (Tazama Manual 412-420). Kazi hizi zote zimegawanyika sehemu kuu tatu.

1. **Kuhubiri na kuongoza ibada**
    - Kuhubiri
    - Ubatizo, Meza ya Bwana, arusi na mazishi
    - Kuongoza kazi za uinjilisti Kanisani

2. **Kuwalinda washirika wa Kanisa**
    - Kuwatembelea washirika
    - Kuwajali wagonjwa na maskini.

- Kuwafariji wenye huzuni (wanaoomboleza).
- Kuwatia moyo watu katika maisha yao ya Ukristo.
- Kuwasaidia wenye dhambi waweze kutubu na kumrudia Mungu.
- Kuwasaidia Wakristo wajazwe na Roho Mtakatifu na waishi maisha ya utakatifu.
- Kuwafundisha na kuwaimarisha Wakristo katika imani yao juu ya Mungu

3. **Kupanga kazi za Kanisa**
   - Kupokea watu kuwa washirika.
   - Kuangalia shughuli za idara tofauti NYI, NMI, Shule ya Jumapili vikundi vya akina mama na kina baba n.k
   - Kuandaa taarifa ya mwaka ya mkutano mkuu wa Kanisa na kutoa taarifa kwa mkutano wa mwaka wa wilaya.

MWITO WA UCHUNGAJI (115-123)

Wakati Kanisa linataka kumuita mchungaji ni lazima lifuate hatua zifuatazo:

1. Wakutane na msimamizi wa wilaya na wachague jina moja kwa Kanisa kulipigia kura. Ni lazima anayeitwa awe kasisi au mtu aliye na cheti cha uchungaji cha wilaya kuwa mchungaji. Hivyo Halmashauri ya Kanisa itajadiliana na msimamizi wa wilaya juu ya yule wanayetaka kumwita. Kura pamoja na mtu huyo ni lazima apate wingi wa kura za halmashauri ya Kanisa. Msimamizi wa wilaya ni lazima amwidhinishe mtu aliyechaguliwa. (115)

2. Jina hilo kisha linawakilishwa kwa washirika wa kanisa na watapiga kura ya “ndiyo” au “hapana”. Ni lazima mtu apate ingalau theluthi mbili za kura ili awe amechaguliwa.

3. Halmashauri ya Kanisa itampa taarifa mchungaji kuwa anaitwa kuwa mchungaji. Ni lazima wamwambie mchungaji watampa mshahara kiasi gani na ni nini matarajio yao kwake. (115.4.)
4. Mchungaji aliyeitwa ni lazima ajibu katika kipindi cha siku 15 (115.1)
5. Wakati mwingine msimamizi wa wilaya na Halmashauri ya Wilaya inaweza kumchagua mchungaji kushika Kanisa la mtaa. Hali hii inaweza ikatokea ikiwa mambo yafuatayo yapo:
    a) Kanisa halijatimiza miaka miwili tangu kuanzishwa.
    b) Kanisa lina wanachama wasiozidi 35.
    c) Wilaya inampa mchungaji sehemu ya mshahara.

KUJIUZULU KWA MCHUNGAJI (120)

Mchungaji anaweza akajiuzulu kutoka kwa kanisa kwa kuandika barua ya kujiuzulu kwa halmashauri ya Kanisa na msimamizi wa wilaya. Ikiwa halmashauri ya kanisa itakubali kujiuzulu kwake na msimamizi wa wilaya kupitisha kwa maandishi, kujiuzulu kwake kutakuwa kumekubaliwa rasmi. Hata hivyo mchungaji ataendelea kuwa mchungaji kwa siku 30 baada ya barua yake kukubali kujiuzulu na halmashauri na msimamizi wa wilaya.

Mchungaji aliyejiuzulu akishirikiana na katibu wa halmashauri ya Kanisa atatayarisha orodha sahihi ya halmashauri wa Kanisa pamoja na anwani zao. Orodha hiyo ni lazima ilingane na ile iliyochapishwa katika taarifa ya mwisho ya mkutano wa wilaya.

Uhusiano wa mchungaji na Kanisa (122)

Kila mwaka mchungaji na halmashauri ya Kanisa watafanya mkutano ambao watahitaji kujichunguza upya matarajio, shabaha na jinsi Kanisa na mchungaji walivyoteleza wajibu wao.

Msimamizi wa wilaya anapaswa kujulishwa mapema na kujichunguza lengo la mkutano huo ni kushughulikia matatizo na tofauti ili kufanya kazi kuzitatua katika hali ya upendo, kukubaliana na kusameheana (121)

Kufanya Upya Kuitwa kwa Mchungaji (123)

Baada ya mchungaji kumaliza miaka miwili ya huduma, kutakuwa na mkutano wa halmashauri ya Kanisa kuangalia upya uhusiano wa mchungaji. Mkutano utasimamiwa na msimamizi wa wilaya au mhudumu aliyewekwa wakfu au muumini aliyeteuliwa na msimamizi wa wilaya. Lengo la mkutano ni kuafikiana bila kufikia kuwango cha halmashauri ya Kanisa kupiga kura rasmi. Ikiwa halmashauri ya Kanisa itafurahia huduma ya mchungaji, basi huduma ya mchungaji itapangwa aendelee kwa miaka mine zaidi.

Halmashauri inaweza kuamua kulipeleka suala hili mbele ya washirika wa Kanisa. Kanisa linaweza kuita mkutano maalum na swali litakuwa "Je, uhusiano wa sasa wa uchungaji utaendelea?" Ikiwa mchungaji hatapata theluthi mbili ya kura basi mchungaji lazima aondoke katika muda utakaokubalika na msimamizi wa wilaya akipata theluthi mbili basi mchungaji ataendelea. (122)

Halmashauri Ya Kanisa (127)

Kila Kanisa lina halmashauri. Wajumbe wa halmashauri ni

1. Mchungaji
2. Msimamizi wa Shule ya Jumapili
3. Mwenyekiti Vijana
4. Mwenyekiti wa NMI
5. Mawakili na wadhamini

Muda wa Mikutano (128)

Mkutano lazima ufanyike kabla ya tarehe 15 ya kila mwezi

Kazi ya Halmashauri ya Kanisa (129-134)

1. Kufanya kazi na mchungaji kuangalia juu ya kazi zote za Kanisa.
2. Kuita mchungaji:
    - Ni lazima wachague mtu na baada ya kupata idhini ya msimamizi wa wilaya watapeleka jina hilo mbele ya mkutano wa Kanisa kwa ajili ya uchaguzi.
    - Kupanga mshahara wa mchungaji kila mwaka

3. Kuchagua
   - Mtunza hazina
   - Katibu wa Kanisa
   - Wajumbe wa kamati ya Uinjilisti na ushirika.
4. Kuhakikisha kuwa bajeti ya wilaya, bajeti ya elimu, na fungu la fedha za Uinjilisti, limelipwa
5. Kuhakikisha kuwa shughuli zote za kifedha zinaangaliwa vizuri na ripoti inatolewa kila mwezi katika mikutano ya kila mwezi ya halmashauri na katika mkutano wa mwaka.
6. Kuchagua watu wawili wa kuhesabu sadaka
7. Kuandaa bajeti ya Kanisa ya mwaka mzima.
8. Halmashauri inaweza kuidhinisha watu wanaoweza kupewa cheti cha Kanisa la mtaa ikiwa Kanisa lina mchungaji ambaye ni kasisi.
9. Kupendekeza kwamba mtu ambaye amekuwa na cheti cha mhudumu cha mtaa apewe cheti cha wilaya.

Katibu wa Kanisa (135)

Kazi ya katibu wa Kanisa ni

1. Kuandika taarifa za vikao vya Kanisa na halmashauri ya Kanisa
2. Kutoa taarifa kwenye mikutano ya Kanisa juu ya shughuli za Kanisa pamoja na idadi ya wanachama
3. Kutunza nyaraka zote za kisheria zinazohusu Kanisa
4. Ikiwa kuna uchaguzi wa mchungaji, katibu atatoa taarifa kwa msimamizi wa wilaya juu ya matokeo ya uchaguzi.

Mtunza Hazina wa Kanisa (136)

Kazi ya Mtunza hazina ni

1. Kupokea fedha ya Kanisa na kulipa baada ya kuidhinishwa na halmashauri ya kanisa kufanya hivyo.
2. Kutunza kumbukumbu za mapato yote na matumizi yote katika vitabu vya fedha.
3. Kutoa ripoti ya fedha kwa halmashauri kila mwezi na katika mkutano wa mwaka wa Kanisa.

Mawakili (137-140)

Kamati ya mawakili itakuwa na wajumbe angalau watatu lakini siyo zaidi ya 13. Kazi ya kamati ni:

1. Kufanya kazi kama kamati ya kukua kwa Kanisa na yenye jukumu la kuwafikia watu, Uinjilisti kujipanua na kuanzisha makanisa mapya
2. Kutoa msaada kwa watu wenye mahitaji, na mahangaiko. Ni lazima wahusike katika kuwapa moyo, kuwatembelea na kuwaangalia wagonjwa na wenye mahitaji na kuhusisha washirika wa Kanisa katika huduma kwa wenye mahitaji katika jamii.
3. Wanaweza kufanya kazi kama kamati ya washirika.
4. Kusaidia katika matayarisho ya meza ya Bwana na kuhudumu katika meza ya Bwana.
5. Pia wanafanya kazi kama kamati ya mawakili wa Kanisa la mtaa na kuwatia moyo watu kutoa kwa ukarimu muda wao, vipawa na fedha kwa kazi ya Mungu.

WADHAMINI (141-144)

Kutakuwa na wajumbe angalau 3 na si zaidi ya 9. Wana jukumu la kutunza viwanja vya Kanisa na majengo ya Kanisa. Wana jukumu la kuhakikisha pesa zinapatikana kwa ajili ya shughuli za Kanisa ikiwa ni pamoja na mshahara ili mchungaji awe huru kutoa muda wake wote kwa kazi za Kanisa.

Halmashauri ya Huduma za Shule ya Jumapili (145)

Katika makanisa ambayo washirika ni chini ya 75, halmashauri ya Kanisa inaweza kufanya kazi kama Halmashauri ya huduma za Shule ya Jumapili Halmashauri ina jukumu la kuangalia kazi za Shule ya Jumapili, kambi za vijana kujisomea Biblia na huduma ya kufundisha katika Kanisa.

Kazi yao ni kuwafikia watu wengi ambao hawajafikiwa kwa ajili ya kuwaleta kwa Kristo na ushirika wa Kanisa. Kuwafundisha neno la Mungu kwa uhakika, kuwafundisha

maadili ya imani ya Kikristo na kuwaendeleza kukua na kuwa kama kristo katika tabia, mtazamo, mazoea, kuwasaidia kuanzisha familia za Kikristo; kuwaandaa waumini kuwa washirika katika Kanisa, na kuwajenga kwa ajili ya kuingia katika huduma mbali mbali za Kikristo.

Chama cha Vijana wa Mnazareti (NYI) (150-151.5)

NYI inafanya kazi katika Kanisa la mtaa katika kuwaimarisha vijana

Lengo la NYI ni:

- Kuwasaidia vijana kumpokea Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi
- Kuwafunza neno la Mungu na maadili ya Kanisa
- Kuwasaidia kukua katika imani ya Kikristo na tabia ya utakatifu
- Kuwasaidia kuwa washirika wa Kanisa na kujishughulisha kwa bidii katika kazi za Kanisa kila mara bila kukosa.
- Kuwaandaa ili waweze kujihusisha katika huduma.

Vijana katika Kanisa la mtaa wanaweza kuchagua baraza likiongozwa na rais, makamu wa rais, katibu na mtunza hazina. Wote hawa lazima wawe washirika wa Kanisa.

Kuna maelezo zaidi katika katiba ya NYI

Jumuiya ya umisheni wa Mnazareti Ulimwenguni (153-155.3) NMI

Jumuiya ya Umisheni wa Mnazareti inafanya kazi katika Kanisa la mtaa kwa kuleta msukumo wa watu wapende maombi na kusaidia kazi ya umisheni katika nchi zingine. Lengo la NMI ni:-

1. Kuwatia moyo washirika wawaombee watu ambao bado hawajampokea Yesu Kristo ili wampokee.
2. Kulijulisha Kanisa kuhusu kazi za Kanisa katika nchi nyingine.
3. Kuwasaidia vijana kusikia wito wa Mungu na hivyo kujitoa kuingia mwenyewe katika huduma.

4. Kuwatia moyo watu kutoa kwa ukarimu kwa ajili ya kazi ya Uinjilisti ulimwenguni.

NMI itakuwa na baraza likiongozwa na rais, makamu wa rais, katibu, mtunza fedha na maofisa wengine kama itakavyoonekana ulazima wake

Maelezo zaidi yapo kwenye katiba ya NMI

VIKUNDI VYA AKINA MAMA NA AKINA BABA

Vikundi vya kina mama na akina baba havikuorodheshwa katika *Kitabu cha Mwongozo (Manual).* Vinatakiwa viundwe kwa njia ile ile kama **NMI** na NYI inavyoundwa. Ni wazo nzuri kwamba mwenyekiti wa akina baba na akina mama wawe kwenye halmashauri ya Kanisa kama ilivyo kwa mwenyekiti wa NYI na NMI.

MUUNDO WA WILAYA

Mkutano mkuu wa wilaya (200-205)

Makanisa ya mtaa ya Mnazareti katika eneo huunganisha pamoja ili kuunda Wilaya. Kuna ngazi tatu tofauti ya muundo wa wilaya katika Kanisa la Mnazareti.

Ngazi ya kwanza -1:

Wakati Kanisa la Mnazareti linaanza katika nchi mpya au eneo jipya ni Ngazi ya kwanza ya wilaya. Mkurugenzi wa jimbo atapendekeza kwa wasimamizi wakuu jina la mtu anayefikiri anafaa kuwa msimamizi wa wilaya. Msimamizi mkuu atamteua msimamizi wa wilaya.

Ngazi ya pili -2:

Ngazi ya 2 ya wilaya ni ile ambayo ina angalau makanisa 10 yaliyoratibiwa na washirika kamili 500 na ina watumishi waliowekwa wakfu watano. Asilimia 50 ya fedha inayohitajika

kwa ajili ya shughuli za kuendesha wilaya ni lazima itoke ndani ya wilaya.

Kiwango cha 2 cha Wilaya	Msimamizi wa Wilaya anaweza kuteuliwa au kuchaguliwa.	
Mahitaji	Makanisa 10 Yaliyoratibiwa	Kasisi 5 Waliowekwa Wakfu
	Washirika 500	Asilimia 50 wanaojitegemea.

Halmashauri ya Wilaya inaweza kuomba kutambuliwa kama Ngazi 2 ya wilaya: Mkurugenzi wa eneo, mkurugenzi wa jimbo na Msimamizi mkuu watatoa pendekezo kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu. Msimamizi wa wilaya anaweza kuchaguliwa.

Ngazi ya tatu-3

Wilaya iliyo katika ngazi ya tatu ni ile ambayo imeonyesha kukomaa kiungozi, kifedha, uaminifu kwa maadili ya Kanisa na maono ya kukua kwa Kanisa ulimwenguni kote.

Wilaya ya ngazi ya tatu ina angalau makanisa 20 yaliyoratibiwa, washirika 1000, watumishi waliowekewa wakfu angalau10, na waweze kujitegemea kwa asili mia moja (100%) katika kuendesha shughuli zote za Wilaya.

Msimamizi wa wilaya atachaguliwa katika mkutano mkuu wa wilaya.

Mkutano mkuu wa wilaya

Wajumbe wa mkutano mkuu wa wilaya ni:-

- Watumishi wote waliowekwa wakfu
- Wachungaji wote wenye vyeti vya wilaya.
- Katibu wa wilaya.
- Mtunza fedha wa wilaya.
- Msimamizi wa huduma za Shule ya Jumapili wa wilaya.
- Mwenyekiti wa vijana.

- Mwenyekiti wa NMI.
- Wasimamizi waliochaguliwa wa Shule ya Jumapili kutoka kila Kanisa la mtaa.
- Mwenyekiti wa vijana aliyechaguliwa na kila Kanisa la mtaa.
- Mwenyekiti wa NMI aliyechaguliwa wa kila Kanisa la mtaa.
- Waumini wajumbe ambao ni washirika wa Halmashauri ya wilaya
- Wajumbe kutoka kila Kanisa la mtaa

Idadi ya washirika	Wajumbe
1-50	wajumbe 2
51-100	wajumbe 3
101-150	wajumbe 4
151-200	wajumbe 5

Hii ina maana kuwa kila Kanisa la mtaa linaweza kutuma wajumbe wafuatao katika mkutano mkuu wa wilaya

1. Mchungaji mwenye leseni ya wilaya au aliyewekwa wakfu.
2. Msimamizi wa Shule ya Jumapili.
3. Mwenyekiti wa vijana.
4. Mwenyekiti wa NMI.
5. Wajumbe waliochaguliwa na Kanisa 2,3,4 na 5 au zaidi ikitegemea ukubwa wa Kanisa kiidadi cha wanachama

Muda wa kufanya mkutano mkuu wa wilaya
Mkutano wa wilaya unafanyika kila mwaka katika wakati/tarehe iliyokubaliwa na msimamizi mkuu.

Kazi ya Mkutano wa Wilaya

Mkutano mkuu wa wilaya husikiliza au kupokea taarifa kutoka:-

1. Watumishi wote waliowekwa wakfu na walio na vyeti vya wilaya

2. Msimamizi wa wilaya
3. Mtunza hazina
4. Halmashauri ya wilaya DAB
5. Mkurugunzi wa elimu ya theolojia
6. Kamati ya elimu
7. Kamati ya halmashauri ya hati za kuhitimu kwa wtumishi.

Mkutano mkuu wa wilaya unawachagua viongozi, na kamati zifuatazo:

- Msimamizi wa wilaya (203.11)
- Halmashauri ya wilaya (203.12)
- Halmashauri ya hati za kuhitimu kwa watumishi (203.15)
- Halmashauri ya mafunzo ya watumishi (203.16, 203.17)
- Kamati ya huduma ya Shule ya Jumapili (203.20, 237)
- Kamati ya mali ya wilaya (203.18)

Mkutano Mkuu wa Wilaya pia Utafanya Yafuatayo:-

- Utatoa vyeti vya wilaya kwa wachungaji (203.2)
- Kuidhinisha wachungaji kuwekwa wakfu (203.6 203.7)
- Kuidhinisha wachungaji kutoka madhehebu mengine kuwa wachungaji katika Kanisa la Mnazareti
- Kuchambua na kudhinisha taarifa ya fedha ya wilaya.

Msimamizi wa Wilaya (206-214.1)

Msimamizi wa wilaya ni lazima awe mtumishi aliyewekwa wakfu. Katika Ngazi ya Kwanza ya wilaya msimamizi wa wilaya anaweza kuteuliwa na msimamizi mkuu. Katika Ngazi ya pili msimamizi wa wilaya anaweza kuteuliwa au kuchaguliwa.

Katika Ngazi ya tatu msimamizi wa wilaya atachaguliwa. Baada ya kumaliza miaka 2, msimamizi wa wilaya anaweza akachaguliwa tena kwa kura ya ndiyo au hapana. Msimamizi wa wilaya lazima apate theluthi mbili (2/3) ya kura ili aweze kubaki katika wadhifa wake huo. Akichaguliwa tena, ataruhusiwa kuhudumu kama msimamizi kwa miaka 4 mfululizo. Ikiwa

msimamizi wa wilaya atajiuzuru au asipochaguliwa kwa kura, ndipo msimamizi mpya atachaguliwa. Katika wilaya iliyo ya Ngazi ya tatu wajumbe wanaweza kumpigia kura mtumishi yeyote katika Kanisa la Mnazareti aliyewekwa wakfu. Wataendelea kupiga kura hadi mtumishi mmoja mwenye kuwekwa wakfu apate theluthi mbili ya kura (2/3).

Katika Ngazi ya pili ya wilaya msimamizi wa atateuliwa na msimamizi mkuu au anaweza kuchaguliwa na mkutano mkuu wa wilaya.

Katika Ngazi ya kwanza msimamizi wa wilaya atateuliwa.

Kazi za Msimamizi wa Wilaya

Kazi za msimamizi wa wilaya zinaweza zikagawanywa katika sehemu kuu mbili.

1. Kufanya kazi na makanisa yote ndani ya wilaya yake
    - Kuongoza, kuimarisha na kuyatia moyo makanisa ya mtaa (208.1).
    - Kukutana na halmashauri za Kanisa la mtaa ili kutathimini kazi za mchungaji (121, 208.3).
    - Kukutana na halmashauri za Kanisa na mchungaji ili kuwapa mwongozo na kuwasaidia kuhusu mambo ya kiroho fedha na mambo ya kiuchungaji (208.3).
    - Kutoa mwongozo na mwelekeo juu ya vituo au makanisa ambayo hayajaratibiwa (208.6).
    - Ikiwa mchungaji hajawekwa wakfu basi msimamizi wa wilaya ataweza kuidhinisha mtu yeyote anayeomba kupata cheti cha Kanisa la mtaa (208.12).
    - Msimamizi wa wilaya anaweza kuwa mchungaji wa Kanisa la mtaa.
    - Msimamizi wa wilaya anaweza kuendesha mkutano wa Kanisa la mtaa.
    - Kuidhinisha maombi ya wachungaji na halmshauri za makanisa ya mitaa kuajiri wasaidizi wenye kulipwa, k.m. mhudumu wa vijana, mchungaji msaidizi n.k

2. **Msimamizi wa wilaya ana majukumu ya kazi zifuatazo katika wilaya**
   - Ni mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya DAB
   - Kuendesha mkutano mkuu wa wilaya ikiwa msimamizi mkuu hayupo.
   - Kuwa mjumbe katika kamati zote za wilaya.
   - Ikiwa kiongozi yeyote katika wilaya atajiuzuru msimamizi wa wilaya anaweza kumteua mtu kuziba nafasi iliyoachwa wazi k.m. katibu, (208.7,) mtunza fedha (208.8).

Katibu wa Wilaya (216-218)

Katibu wa wilaya anachaguliwa na Halmashauri ya wilaya ya DAB na atatumikia nafasi hii kwa miaka 1-3 na anaweza akachaguliwa tena.

Kazi za katibu ni

1. Kuandika kwa usahihi na kuzitunza kumbukumbu za mkutano mkuu wa wilaya
2. Kuweka kwa usahihi kumbukumbu za takwimu zinazohusu wilaya.
3. Kupeleka nakala ya ripoti ya wilaya kwenye ofisi ya eneo.
4. Kutunza nyaraka zote za kisheria zinazohusu wilaya.

Mtunza Hazina (219-220.2)

Mtunza hazina atachaguliwa na halmashauri ya wilaya (DAB). Mtunza hazina wa wilaya atafanya yafuatayo:

1. Kupokea fedha zote zinazoingia wilayani na kulipa fedha kulingana na maelezo na taratibu zilizowekwa na halmashauri ya wilaya na mkutano mkuu wa wilaya.
2. Kuweka kumbukumbu safi na sahihi za fedha zinazopokelewa na kutumika na kutoa ripoti kila mwezi kwa msimamizi wa wilaya na kutoa ripoti ya mwaka kwa mkutano mkuu wa wilaya

Halmashauri ya Wilaya (221-225)

Wajumbe wa kamati hii huchaguliwa kila mwaka wakati wa mkutano mkuu. Wajumbe wa kamati hii ni

- Msimamizi wa wilaya
- Watumishi hadi watu waliowekwa wakfu.
- Washirika wa kanisa angalau watatu.

Katika wilaya ambayo ipo ngazi 1 na 2, mkurugenzi wa eneo anaweza kumteua mmisionari kuwa mwakilishi katika halmashauri ya wilaya DAB.

KAZI YA HALMASHAURI YA WILAYA NI:-
Masimamizi wa wilaya (DS) ni mwenyekiti wa DAB.

1. Kuweka muda wa kuanza na kumalizika kwa mwaka wa fedha wa wilaya.
2. Wajumbe watashauriana na msimamizi wa wilaya kuhusu wahudumu na makanisa ya mtaa katika wilaya. Pia watatoa ushauri kuhusu kamati yoyote ya wilaya.
3. Kumchagua mtunza fedha na katibu.
4. Ikiwa mchungaji ana cheti cha wilaya na ni mchungaji halmashauri ya wilaya, itapendekeza apewe cheti kingine kwa mwaka mwingine.
5. Ikiwa mtu ye yote ataleta tuhuma juu ya utovu wa nidhamu, Halmashauri ya wilaya DAB itateua kamati ya watu 3 au zaidi waliowekwa wakfu kuchunguza tuhuma zilizoletwa
6. Halmashauri ya Kanisa ina majukumu ya kuangalia mali zote na majengo ya Kanisa katika wilaya
7. Ikiwa mchungaji kutoka dhehebu jingine atapenda kujiunga na Kanisa la Mnazareti vyeti vyake vitachunguzwa na halmashauri ya wilaya na kama wakimkubali na kumpitisha mchungaji huyo atapokelewa katika ushirika wa Kanisa.

Halmashauri ya Hati za Kuhitimu kwa Watumishi (226-228.10)

Kamati hii ina wajumbe wasiopungua 5 na wasiozidi 15. Msimamizi wa wilaya ni mjumbe wa kamati hii na wajumbe wengine huchaguliwa kwa muda wa miaka minne. Msimamizi wa wilaya ni mwenyekiti wa kamati hii isipokuwa kama ameomba kamati kumchagua mtu mwingine awe mwenyekiti. Kamati itamchagua katibu ambaye ataandika kwa usahili kumbukumbu na maamuzi yote yaliyofanywa na kamati.

Kazi ya Kamati ni:

1. Ni lazima wamchunguze kila mtu anayeomba kupata cheti cha wilaya au kuwekwa wakfu.
2. Wataangalia kwa uangalifu ujuzi wa mtu katika maisha ya wokovu, ujuzi wa utakatifu wa moyo, kujazwa roho mtakatifu, maarifa juu ya Biblia, maadili ya Kanisa. Jinsi anavyokubali kanuni za mwongozo wa Kanisa, ushahidi wa vipawa vya kiroho, tabia yake na jinsi anavyoweza kukaa katika huduma
3. Kama mtu alikuwa na cheti cha Kanisa la mtaa na ametumika kama mchungaji wa Kanisa la mtaa, kamati hii ni lazima impitishe kuendelea kuwa mchungaji.

Halmashauri ya Mafunzi ya Watumishi ya Wilaya (229-231.4)

Kutakuwa na wajumbe 5 au zaidi ambao ni watumishi waliowekwa wakfu katika kamati hii. Kamati hii itachaguliwa wakati wa mkutano mkuu na watafanya kazi hii miaka 4.

Kamati itamchagua mwenyekiti na katibu. Kazi ya kamati hii ni kufuatilia masomo na mipango ya wale wanaojiandaa kuwekwa wakfu. Wanatakiwa wawatie moyo, kuwaongoza na kuwasaidia katika kuwafunza kwa kufuata ratiba ya masomo kwa wale wanaosoma.

Kamati ya Mali ya Kanisa (234-235)

Kamati ya mali ya Kanisa itajumlisha msimamizi wa wilaya, wajumbe 2 waliowekwa wakfu na wajumbe wawili washirika wa Kanisa. Wajumbe wanaweza kuchaguliwa kwa miaka 4.

Halmashauri ya wilaya (DAB) inaweza kufanya kazi kama kamati ya mali ya Kanisa pia. Kazi ya kamati ya mali ya Kanisa ni kutoa ushauri kwa msimamizi wa wilaya na makanisa ya mtaa kuhusu mambo yanayohusu aridhi (kiwanja) ramani za majengo, na mipango ya ujenzi. Ramani yo yote ya Kanisa ni lazima ipitishwe na msimamizi wa wilaya na kamati ya mali ya Kanisa kabla ya ujenzi kuanza.

Kamati ya Huduma ya Shule ya Jumapili (237-238.3)

Kamati hii itakuwa na wajumbe wafuatao

- Msimamizi wa wilaya (DS)
- Mwenyekiti wa NMI
- Mwenyekiti wa vijana (NYI)
- Mwenyekiti wa wilaya ya shule ya jumapili na wajumbe 3 wa kuchaguliwa

Mara tu baada ya mkutano mkuu wa wilaya, watakutana na kuwachagua wafuatao

- Katibu
- Mtunza hazina
- Mkurugenzi wa huduma watu wazima
- Mkurugenzi huduma ya watoto
- Hawa watakuwa wajumbe wa kamati ya wilaya ya huduma ya shule ya jumapili. Kamati ni lazima isimamie kazi zote za shule ya Jumapili katika wilaya.

KIKAO KIKUU

Kikao kikuu, ni mkutano muhimu sana kwa Kanisa la Mnazareti. Kikao hiki ndicho chenye mamlaka ya kutayarisha mafundisho ya imani ya Kanisa la Mnazareti na kutunga sheria za kuliongoza Kanisa ulimwenguni kote. Wasimamizi wakuu ndio watakaokuwa wenyeviti wa kikao hicho.

Wajumbe wa kikao kikuu ni (301):

1. Wajumbe watachaguliwa na mkutano wa wilaya wa mara kwa mara (Ngazi ya tatu), nusu yake watakuwa wajumbe na nusu wahudumu waliowekwa wakfu.

Idadi ya washirika	Wajumbe/Wahudumu	Wajumbe
1- 2,000	Msimamizi wa wilaya	1
2,001-5,500	Msimamizi +1	2
5,001-9,000	Msimamizi + 2	3

2. Wilaya ya Ngazi ya 2 inaweza kutuma msimamizi wa wilaya na muumini mmoja.
3. Wilaya ya ngazi ya 1 inaweza kutuma msimamizi wa wilaya lakini hawezi kupiga kura katika kikao.
4. Wasimamizi wakuu wote.
5. Katibu mkuu.
6. Mtunza hazina mkuu.
7. Mhariri wa gazeti la "Utakatifu Leo" (Holiness Today).
8. Rais wa vijana ulimwengu.
9. Rais wa NMI ulimwengu.
10. Wakurugenzi wa majimbo.

Wakati wa Mkutano (302)

Kikao kikuu kitafanyika mwezi Juni kila baada ya miaka 4 km 2005, 2009, 2013, 2017 nk

Kasi ya Kikao Kikuu (305)

1. Kuwachagua wasimamizi wakuu 6 kwa kura ya 2/3.
2. Kuchagua wajumbe wa Kamati Kuu

Wilaya zinaweza kutuma mapendekezo kuhusu mabadiliko wanayotaka yafanyike kwenye katiba (Manual). Mapendekezo haya yatapelekwa kwenye kamati zao. Kikao kikuu kwa ajili ya majadiliano. Kamati zitafanya mapendekezo kukubali au kuyakataa na baadaye kuyapeleka kwenye kikao kikuu ambapo pia kitayajadili na baadaye kuyapigia kura. Hii ndiyo njia pekee

ambayo inaweza kuleta mabadiliko au marekebisho katika Manual ya Kanisa.

Wasimamizi Wakuu (306-307.14)
Wasimamizi wakuu 6 ni lazima wawe wahudumu waliowekwa wakfu. Ni lazima wawe zaidi na umri zaidi ya 35 na isizidi miaka 68. Hawa wanachaguliwa na kikao kikuu. Kazi yao ni kama ifuatavyo-:

1. Kufanya usimamizi wa kijumla wa kazi ya Kanisa la Mnazareti ulimwenguni kote.
2. Ni wenyeviti wa shughuli zote za kikao kikuu.
3. Wanafanya kazi kusaidia wilaya.
   Wanakuwa wenyeviti wa mikutano ya wilaya au kumchagua mtu mwingine badala yao.
   Kuweka wakfu wale waliochaguliwa na mkutano wa wilaya kuwa wahudumu kama makasisi au wanaweza kumchagua mwingine kufanya kazi badala yao.

Wanaweza kuteua mtu kuwa msimamizi wa wilaya ikiwa kutatokea nafasi baada ya mkutano mkuu wa wilaya. Watafanya hivyo wakishauriana na Halmashauri ya wilaya (DAB), Mwenyekiti NMI, NYI na mwenyekiti wa Shule ya Jumapili, katibu wa wilaya na mtunza hazina wa wilaya (Tazama 207).

Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu (315-324)
Halmashauri ya wasimamizi wakuu itakutana kila baada ya miezi mitatu.

1. Kutoa usimamizi kwa kazi ya Kanisa ulimwenguni. Kanisa la ulimwengu limegawanywa katika majimbo sita ya kimataifa na kila jimbo linapewa msimamizi mmoja.
2. Kuangalia shughuli zote za Kanisa na idara zake.
3. Wasimamizi wakuu na Halmashauri ya wasimamizi wataamua jinsi mfuko wa kimataifa wa uinjilisti utakavyotumika.

4. Halmashauri ya wasimamizi wakuu ina mamlaka ya kutafsiri sheria na mafundisho makuu ya Kanisa la Mnazareti.
5. Ikiwa mtu ameachwa na mke au mume na kupewa talaka na mtu huyo anataka kuwekwa wakfu, ni lazima apate kibali na Halmashauri ya wasimamizi wakuu.
6. Wanaweza kufanya jambo lolote wanaloona ni la lazima ikiwa litasaidia kazi ya Kanisa na ili mradi tu jambo hilo haliendi kinyume na sheria za Kanisa la Mnazareti.

Katibu Mkuu (325-328.1)
Katibu mkuu huchaguliwa na Halmashauri kuu. Katibu mkuu anawajibika kwa Halmashauri ya wasimamizi wakuu na Halmashauri kuu.
Kazi ya katibu mkuu ni

1. Kuandika kwa usahihi taarifa ya mambo yanayofanyika katika mkutano mkuu wa kikao kikuu na Halmashauri kuu.
2. Kuandika kwa usahihi takwimu za washirika wa Kanisa.
3. Kuhifadhi kwa uangalifu hati zote za kisheria na hati zingine muhimu za Kanisa.

Mtunza hazina mkuu (329-330.7)
Mtunza hazina mkuu anachaguliwa na Halmashauri kuu. Mtunza hazina mkuu atawajibika kwa Halmashauri ya Wasimamizi Wakuu na Halmashauri Kuu.
Kazi za mtunza hazina mkuu ni

1. Kutunza fedha zote zinazopokelewa katika Kanisa.
2. Kulipa fedha kulingana na maagizo ya Halmashauri kuu.
3. Kutoa ripoti ya fedha za Kanisa kwa Halmashauri kuu kila mwisho wa mwaka wa fedha.

Halmashauri Kuu (331-336)
Halmashauri kuu inachaguliwa na kikao kikuu. Mtunza hazina mkuu na katibu mkuu ni Wajumbe wa Halmashauri hii kwa

wadhifu wao. Kuna wajumbe kama 40 katika halmashauri na hukutana mara moja kwa mwaka.

Wilaya mbali mbali zinaunda majimbo. Kila jimbo linaweza kuteua waumini na wahudumu waliowekwa wakfu kuingia katika halmashauri hii. Halafu kati ya wajumbe hao huchaguliwa kuingia kwenye kikao kikuu kutoka majimbo.

Wajumbe wa Halmashauri Kuu

Ukubwa wa jimbo	Waumini	Wahudumu
Mpaka 100,000	1	1
100,001 - 200000	2	2
Zaidi ya 200,000	3	3

Rais wa NYI ulimwengu	Mshirika 1	
Rais wa NMI ulimwengu	Mshirika 1	
Vyuo vya Mnazareti	1	1

Kazi ya Halmashauri Kuu

Halmashauri Kuu inaangalia kazi zote za Kanisa ulimwenguni. Inasaidia kila idara za Kanisa kufanya kazi kwa ushirikiano na idara zingine kwa amani na utulivu.

Halmashauri Kuu ndiyo inayoamua jinsi fedha au mfuko wa uinjilisti ulimwenguni utakavyotumika. Inapanga matumizi ya fedha kwa idara mbali mbali na taasisi za Kanisa. Halmashauri kuu hupokea na kusikiliza ripoti kutoka idara zote za Kanisa.

Utumishi Katika Kanisa la Mnazareti

Kuna ngazi tatu za utumishi katika Kanisa la Mnazareti

1. Mtumishi katika Kanisa la Mtaa aliyeidhinishwa na halmashauri ya Kanisa la mtaa.
2. Mtumishi mwenye cheti cha wilaya kilichoidhinishwa na mkutano mkuu wa wilaya.
3. Kasisi au Shemasi ambaye ameidhinishwa na mkutano wa wilaya na pia amewekwa wakfu.

Mhudumu wa Cheti cha Kanisa la Mtaa 428

1. Mhudumu wa Kanisa la mtaa lazima awe mshirika wa Kanisa la Mnazareti. Mhudumu wa mtaa anapewa cheti na halmashauri ya Kanisa na hufanya kazi chini ya uongozi, uangalizi wa mchungaji. Hii humpa nafasi nzuri mhudumu kutumia na kuendeleza vipawa vya kiutumishi. Hapa mhudumu ameingia katika safari ndefu ya kujifunza.

2. Ikiwa mchungaji wa Kanisa la mtaa ni Kasisi, Halmashauri ya Kanisa la mtaa itatoa cheti kilichosainiwa na katibu na mchungaji.

3. Ikiwa mchungaji wa Kanisa la mtaa hakuwekwa wakfu itabidi mchungaji na halmashauri ya Kanisa la mtaa wapeleke mapendekezo kwenye halmashauri ya wilaya ambayo itaidhinisha ikifuata maelekezo ya msimamizi wa wilaya.

4. Mtu anayehitaji kuwa mhudumu wa Kanisa la mtaa atachunguzwa kuhusu ujuzi wake juu ya wokovu, elimu ya mafundisho ya Biblia, na Manual ya Kanisa. Ni lazima aonyeshe kuwa anavyo vupawa muhumu vya kiroho na kukua kiroho.

5. Cheti kitatolewa kwa muda wa mwaka mmoja.

6. Mhudumu wa mtaa atafanya kozi ya masomo ya utumishi. Ikiwa baada ya miaka miwili hajamaliza masomo hatapewa cheti mara nyingine.

7. Cheti kitatolewa tena na Halmashauri ya Kanisa la mtaa baada ya kupendekezwa na mchungaji. Ikiwa mchungaji hajawekwa wakfu, idhini iombwe kutoka kwa msimamizi wa wilaya ambaye ndiye ataidhinisha.

8. Mhudumu wa cheti cha Kanisa la mtaa haruhusiwi kuendesha meza ya Bwana, ubatizo na kufungisha ndoa.

Mhudumu Aliyepewa Cheti Cha Wilaya (429)

1. Wanaoomba ni lazima wawe washirika wa Kanisa la Mnazareti na ni lazima wawe na mwito wa kuhudumu katika maisha yao.
2. Anayeomba lazima awe na cheti cha Kanisa la mtaa kilichokaa kwa mwaka mmoja
3. Anayeomba lazima aidhinishwe na halmashauri ya Kanisa ambalo ni washirika. Ikiwa anayeomba anachunga Kanisa ni lazima maombi yake yapitishwe na halmashauri ya wilaya (DAB).
4. Anayeomba ni lazima awe amemaliza masomo katika chuo cha Biblia kwa mwaka mmoja au amemaliza angalau msomo 8 katika mpango wa masomo ya uhudumu.
5. Mwombaji lazima ajaze kwa uangalifu fomu ya maombi na aipeleke kwa Halmashauri ya hati za kuhitimu kwa wahudumu.
6. Mwombaji lazima ahudhurie madarasa yanayotoa kozi za uhudumu na wilaya au chuo cha Biblia.
7. Ikiwa anaongoza Kanisa, mchungaji lazima apeleke taarifa kila mwezi kwa Msimamizi wa wilaya.
8. Anayeomba ataulizwa maswali na Halmashauri ya hati za kuhitimu kwa wahudumu kuweza kuamua kama anayeomba amekua kiroho, kiakili na kama anafaa katika kazi ya uhudumu.
9. Anayeomba ni lazima apate au akubaliwe kwa kura nyingi katika mkutano mkuu wa wilaya.
10. Cheti kinaisha kila baada ya mwaka mmoja.
11. Wahudumu wanaopewa cheti na ni wachungaji na wamefaulu kozi zinazotakiwa, wana uwezo wa kuhubiri na kuadhimisha sakramenti katika ushirika wao wa Kanisa.

12. Wahudumu wengine kutoka madhehebu ya kiinjilisti lazima waonyeshe vyeti vyao na ikiwa wamesoma masomo yanayolingana na yale ya Kanisa la Mnazareti na wametimiza masharti yaliyoonyeshwa hapo juu wanaweza kupewa cheti cha wilaya.`

Cheti cha wilaya kikishatolewa mchungaji lazima atimize masharti yafuatayo ili aweze kupewa cheti mwaka unofuata

1. Mchungaji lazima ajaze fomu ya kuomba upya cheti.
2. Mchungaji lazima apitishwe na halmashauri ya wilaya.
3. Mchungaji lazima awe amemaliza ingalau masomo mawili au zaidi katika kozi
4. Ikiwa anachunga Kanisa ni lazima apeleke taarifa (ripoti) kila mwezi kwa msimamizi wa wilaya.
5. Mchungaji lazima aonyeshe kuwa na neema, vupawa na kufaa kwa kazi ya Mungu.
6. Mchungaji lazima aidhinishwe na Halmashauri ya hati za kuhitimu kwa wahudumu na halmashauri ya wilaya.

7. Mchungaji lazima awe na lengo la kuwekwa wakfu kama kasisi au shemasi katika Kanisa la Mnazareti. Mhudumu aliyepewa cheti cha wilaya hawezi kupewa cheti hicho ikiwa amekaa nacho kwa miaka 10 isipokuwa kwa sababu maalumu.

Shemasi (430)
Shemasi ni mtu ambaye anasikia wito wa kutumika katika huduma ya Kikristo lakini si kuhubiri. Mashemasi wengine wanafanya kazi kama za kuhudumia watoto,
Kufanya kazi huduma za Kikristo mahospitalini, wengine kuwatembelea watu au wengine wanajishughulisha na huduma ya kuwaonea watu huruma.
Shemasi anapewa uwezo wa kushirikisha sakramenti zote zinazotambuliwa na Kanisa, na wakati mwingine kuongoza ibada na kuhubiri.

Hatua za kuwa shemasi ni sawa na zile za mtu aliyewekwa wakfu isipokuwa tofauti ni kwenye masomo yanayohitajika.

Kasisi (431)
Nafasi ya kasisi ni kwa wale ambao wana wito ulio wazi wa kuhubiri Neno la Mungu. Anayetaka nafasi hii lazima amalize kozi ya masomo yanayotambulika kumtayarisha kuwa mhudumu. Mtu huyu lazima aonyeshe kukomaa kiroho, vipawa na matunda ya roho katika huduma yake. Inatazamiwa kuwa mtumishi aliyewekwa wakfu atatumia nguvu zake kwa muda wote katika kuudumia shughuli za Kanisa. (Kikristo). Hii ni nafasi ya kudumu na kuwekwa wakfu hakufanywi mwaka hadi mwaka.

Mtumishi mwenye cheti cha wilaya ni lazima atimize masharti yafuatayo ili aweze kuwekwa wakfu.

1. Amalize masomo yote katika kozi husika kwa kujiandaa kuwekwa wakfu.
2. Awe amehudumu kama mhudumu mwenye cheti kwa miaka miwili mfululizo au miaka miwili mfululizo au miaka mitatu kama mchungaji msaidizi.
3. Ni lazima awe amependekezwa kupata cheti na halmashauri ya Kanisa au halmashauri ya wilaya (DAB).
4. Ni lazima awe amechunguzwa na kupitishwa na Halmashauri ya hati za kuhitimu kwa wahudumu kwamba awekwe wakfu.
5. Kama mtu amepewa talaka, halmashauri kuu ya wasimamizi wataamua kama mtu huyo awekwe wakfu au la.
6. Apitishwe kwa kura ya theluthi mbili na mkutano mkuu.
7. Ibada ya kuwekwa wakfu ni ibada maalumu inayoendeshwa na msimamizi mkuu katika mkutano mkuu wa wilaya. Msimamizi mkuu pamoja na watumishi wengine waliowekwa wakfu, wataweka mikono kwa mtumishi na kumweka wakfu kama kasisi katika Kanisa la Mnazareti.

Kutambuliwa kwa Hati za Kuhitimu (432)
Wahudumu wengine kutoka madhehebu mengine ya kiinjili wanaopenda kujiunga na Kanisa la Mnazareti ni lazima wafuate hatua zifuatazo.

1. Wafaulu mtihani juu ya Manual na historia ya Kanisa la Mnazareti.
2. Wajaze karatasi ya Maombi ya Watahiniwa wa Kuwekwa Wakfu na Makasisi Wakiomba Kutambuliwa kwa Vyeti Vyao.
3. Watimize masharti yote yanayomhusu kasisi

Msimamizi mkuu atatoa cheti cha kumtambulisha

Kujiuzulu au kuondolewa kutoka katika huduma.
Cheo cha kasisi ni cha kudumu kwa maana kwamba hakitolewi kila mwaka, bali anatakiwa kutoa ripoti/taarifa kila mwaka katika mkutano mkuu wa wilaya.

Cheti cha kuwekwa wakfu ni kama mkataba kati ya mhudumu na Kanisa la Mnazareti. Mkataba huu utaheshimika/utakuwa na nguvu wakati wote wa maisha ya mhudumu ikiwa mafundisho yake yatakuwa sawasawa na mafundisho na taratibu za Kanisa.

Watumishi waliowekwa wakfu hawatafanya shughuli za mara kwa mara ambazo ni nje ya maelekezo ya Kanisa la Mnazareti bila kupewa kibali cha maandishi na Halmashauri ya wilaya (DAB). Ikiwa kasisi au shemasi atajiunga na dhehebu jingine basi atasimama kuwa kasisi au shemasi katika Kanisa la Mnazareti (433.10)

Mtumishi aliyewekwa wakfu anaweza kujiuzulu na akarudisha vyeti vyake kwa wilaya, ambao watavituma kwa katibu mkuuu kwa ajili ya kuvitunza. (435.1)

Mhudumu ambaye atabakia bila kupangiwa kazi kwa zaidi ya miaka mine, atawekwa kwenye orodha ya watu waliojiuzulu katika kumbukumbu za halmashauri ya wilaya. (436.2)

Taratibu za kushughulikia mtumishi ambaye ametuhumiwa na makosa ya utovu wa tabia isiyoridhisha zimeorodheshwa katika Manual (505-507.2).

Neno la Mungu kwa Wachungaji na Viongozi wa Makanisa

Mtume Paulo aliwaambia viongozi katika Kanisa la Efeso "Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha Kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe".

Matendo ya Mitume 20:28

Mtume Petro alisema "Lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo, si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo, wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao bali kwa kujifanya vielelezi kwa lile kundi. Na mchungaji mkuu atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka".

1 Petro 5:2-4


Eglise du Nazaréen
Kanuni za Imani
Mungu wa Utatu
1
2
3
Yesu Kristu
Roho Mtakatifu
4
Maandiko Matakatifu
Upatanisho
6
7
5
Zambi ya Asili na binafsi
Neema inayo Tanguliya Wokovu
8
Toba
Kuhesabiwa haki Kuhuishwa Kufanywa wana
9
10
Utakaso kamili
Kanisa 11
12
Ubatizo
13
Meza ya Bwana
14
Uponyaji wa Mungu
15
Kuja kwa pili kwa Kristu
16
Ufufuo, Hukumu, Kikomo

ANP
Africa Nazarene Publications